

**Kigogo** wa CWT mbaroni madai ya kufanya fujo

UKURASA 3



**Wasiojulikana** wadaiwa kubaka, kunyonga mtu

UKURASA 3

**Biashara** ya nyama ya punda sasa yafanywa kwa kificho

UKURASA 5

**KLOPP: ALONSO KOCHA BORA WA KIZAZI KIPYA**

UKURASA 21

Jumapili Februari 18, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581590

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

# MWISHO WA ENZI

• **Lowassa** azikwa, Samia aongoza mamia, Malasusa, maaskofu 12 wahudhuria... *Endelea Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua kwenye kaburi la Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa, baada ya maziko yake, nyumbani kwake, Monduli, mkoani Arusha jana. Picha ndogo: Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa (kushoto), akiwaongoza maaskofu wenzake katika maziko hayo na Wazee wa Kimaasai (Leigwanani), wakitoa baraka zao za mwisho. **Picha zaidi Uk. 8. PICHA ZOTE: GETRUDE MPEZYA**

## Simulizi Askofu aliyewasema viongozi wa serikali bila woga



UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA HAIKAMATIKI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Viongozi mbalimbali wa kitaifa, wakiwa kwenye maziko ya Hayati Edward Ngoyai Lowassa nyumbani kwake, Monduli mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Mwisho wa enzi, Lowassa azikwa

**Na Allan Isack,** MONDULI

NI mwisho wa enzi. Ndivyo inavyosadifu katika hali halisi ya sasa baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, kuzikwa rasmi jana nyumbani kwake, Kijiji cha Ngarash, Monduli mkoani Dodoma.

Wakati wa maziko hayo yaliyofanyika kidini, kiserikali na kimila, nchi ilisimama kutokana na Watanzania wengi kushuhudia tukio hilo la kumweka kiongozi huyo aliyejipatia umaarufu kemkem enzi za uhai wake hasa alipokuwa katika uongozi kwenye nafasi mbalimbali.

Mwili wa kiongozi huyo ulishuhudiwa ukishushwa taratibu kaburini, huku waombolezaji waliokuwa eneo hilo wakionekana kushikwa na huzuni na wengine kububujikwa na machozi.

Uchungu zaidi ulikuwa kwa familia yake ikiongozwa na mkewe, Regina Lowassa, ambaye wakati mwili ukishushwa kaburini na maofisa waandamizi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wenye cheo cha Kanali, alikuwa amejifunika kijitabu cha ratiba ya maziko.

Wakati mama akiwa katika hali hiyo, watoto wake walionekana kububujikwa na machozi na kujifuta ikiwa dhahiri kwamba hawatamwona tena mpendwa wao kwa kuwa ameshawekwa katika nyumba yake ya milele.

Katika maziko hayo, kulikuwa na matukio matatu, la kwanza lilikuwa nusu gwaride la wanajeshi wa mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan. Wakati mwili ukiingizwa kwenye eneo la hafla ya mazishi, maofisa wa JWTZ wenye vyeo vya Meja. Walibeba jeneza lenye mwili wakiwa wasaidizi wa makanali.

Tukio la pili lilikuwa kupigiwa mizinga 17 iliyopigwa angani na wanajeshi wa JWTZ ikiwa ni utaratibu wa maziko ya kiongozi wa ngazi ya juu kitaifa. Tukio lingine lilikuwa kufanyika kwa ibada tatu tofauti za ibada ya kimila, kiserikali pamoja na ya kidini.

Aidha ibada ya kidini iliongozwa na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa. Lowassa alikuwa muumini wa kanisa hilo.

Mbali na Malasusa ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, maaskofu wengine wa kanisa hilo waliokuwapo na dayosisi zao kwenye mabano ni Dk. Fredrick Shoo (Kaskazini), Dk. Msafiri Mbilu (Kaskazini Mashariki),

Chediel Sendoro (Mwanga), Dk. Benson Bagonza (Karagwe), Dk. Abel Mollel (Kaskazini Kati), Charles Mjema (Pare), Dk. Solomon Masangwa (mstaafu Kaskazini Kati), Nicholous Nsanganzelu (Mbulu) na Jacob Mameo ole Paulo (Morogoro). Pia Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, Isaack Aman, alihudhuria.

**VIONGOZI WA SERIKALI**

Mbali na Rais Samia, viongozi wengine wa kitaifa waliokuwapo katika maziko hayo ni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka.

Wengine ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Dk. Doto Biteko, na mawaziri wakuu wastaafu, Mizengo Pinda na Fredrick Sumaye.

Pia alikuwepo Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, Katibu Mkuu wa CCM. Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu na manaibu makatibu wakuu na magavana kutoka Kenya.

Rais Samia alifika katika maziko hayo saa 4:30 asubuhi, huku mwili wa Lowassa ukipelekwa eneo lililopangwa kwa ajili ya kufanyia ibada saa 5: 30 asubuhi.

**KAULI YA MALASUSA**

Akizungumza wakati wa mahubiri katika ibada ya maziko, Askofu Malasusa alisema kifo cha Lowassa kimeleta huzuni kwa familia na taifa kwa ujumla.

"Kifo kinaleta huzuni, ni katili sana na kinatisha. Hakuna anayetamani kufa kwa kuwa madaktari huwa wanajaribu kutibu ili mwanadamu aendelee kuishi lakini haiwezekani kuishi hapa duniani milele.

"Hakuna binadamu anayetamani kutangulia kufa kwa kuwa kifo kina tisha na biblia imeeleza kuwa binadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi," alisema Malasusa.

Askofu Malasusa alisema uhai wa binadamu uko mikononi mwa Mwenyezi Mungu, hivyo kwa kuwa siku za kuishi duniani ni chache na saa haijulikani ya kutwaliwa aliwataka wananchi kujiandaa.

Wakati wa ibada ya kimila, Kiongozi Mkuu wa Malaigwanani Tanzania, Isack Ole Kisongo, alisema wamefanya dua ya kimila ya kumwombea Lowassa kwa kuwa alikamilisha taratibu zote za kuwa kiongozi wa kimila (Laigwanani).

Alisema dua hiyo ya kawaida haiwezi kuingiliana na ya dini na kama isingekuwa hivyo wangepaswa kumpaka mafuta marehemu na watoto wake wa kiume kwenye paji la uso.

# Samia asema umaarufu wake uliibeba Chadema

**Na Allan Isack,** MONDULI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilipata wabunge 115 na madiwani wengi kwa sababu ya umaarufu na kukubalika kwa Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa.

Lowassa aliyefariki dunia Jumamosi iliyopita katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam, alizikwa jana nyumbani kwao, Monduli mkoani Arusha.

Akizungumza jana katika maziko ya kiongozi huyo, Rais Samia alisema idadi hiyo ilichangiwa na mambo mengi na mzuri aliyofanya (Lowassa) kwenye jamii na kwa taifa kwa ujumla.

Aliyasema hayo baada kuibuliwa hoja na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, kwamba haiwezekani kuitenga, kuandika au kurekodi mazuri aliyoyafanya Hayati Lowassa pasipo kukitaja chama hicho cha upinzani.

Mbowe alisema taifa limepoteza mmoja wa viongozi mahiri, mpenda maendeleo, mwana mageuzi na kipenzi cha watu wengi na alitoa pole kwa familia na wananchi na Watanzania kwa msiba huo.

Samia alisema: "Wasifu wa Lowassa alishika nyadhifa mbalimbali ndani ya chama na serikalini hadi kufikia nafasi ya Waziri Mkuu na nusu ya maisha yake ametumia katika utumishi na uongozi wa umma. Alijitolea muda wa maisha yake kwa ajili ya nchi yake kwa kubeba dhamana kwa kila sehemu alipokabidhiwa.

"Lowassa alikuwa kiongozi mlezi ambaye aliwalea vijana wengi kwenye siasa ambao kwa sasa wanaendelea kulitumikia taifa na sifa hii ya ulezi kwa vijana ilimjengea umaarufu na mapenzi makubwa kwa wananchi Ndiyo maana alichosema hata mdogo wangu Freeman Mbowe yale matokeo ya zile kura ni kwa sababu ya Lowassa ambaye alijenga umaarufu mkubwa sana yeye mwenyewe binafsi na siyo chama chao, ndiyo sababu umekuja na kupata kitu cha kusema".

Alisema Lowassa alipokuwa mgombea wa urais mwaka 2015 aliweka wazi kwamba kipaumbele chake cha kwanza kilikuwa elimu, pili elimu na cha tatu elimu kwa sababu alipenda vijana wapate elimu, maarifa na ujuzi kwa ajili ya ustawi wa familia zao na jamii kwa ujumla.

"Lowassa alikuwa muumini wa elimu kama nyenzo ya kujikomboa na umasikini na mara zote alisisitiza kuwa haupendi umasikini, nakumbuka aliwahi kusema nimekuwa na nitaendelea kupambana na kusisitiza elimu bora ambayo inawaandaa vijana kuingia kwenye soko la ajira," alisema Samia.

Pia alisema imani na msimamo wa Lowassa vilisukuma na kusimamia kwa mafanikio mpango wa maendeleo wa elimu ya sekondari akiwa Waziri Mkuu.

Alisema mpango huo ulianza kuongeza wanafunzi wanaopata elimu ya sekondari kwa utaratibu sambamba na kusimamia ujenzi wa shule za sekondari katika kila kata nchini, licha ya kuwapo kwa maoni kinzani kutoka kwa baadhi ya wadau wa elimu.

Vilevile alisema Lowassa alikuwa kiongozi jasiri, shupavu na mstahimilivu na mlezi kwa kila jambo alilokuwa akifanya wakati akiwa serikalini na kwenye CCM.

"Ndugu yetu Lowassa alikuwa kiongozi jasiri na shupavu na alionyesha ushupavu katika nyakati mbalimbali wakati wa uongozi wake kwa kuwa alisimamia mambo yaliyokubalika ndani ya serikali na yale aliyoagizwa na chama bila kutetereka. Mfano alipokuwa Waziri wa Maji na Uvuvi licha ya kuwapo kwa shinikizo la kutokutumia maji ya Ziwa Victoria kwa sababu za kihistoria kwa ujasiri na ushupavu alishauri vema serikali," alisema.

Sambamba na hayo, alisema pia alisema Hayati Lowassa atakumbukwa kwa usimamizi na ufuatiliaji wa mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa zilizoleta mapinduzi katika utoaji wa huduma za maji safi na salama na uondoaji wa maji taka.

"Jambo la kujifunza ukipewa dhamana ya uongozi au kuaminiwa katika nafasi mbalimbali ni lazima tuwe na uthubutu na ubunifu pamoja na kusimamia na kutekeleza maelekezo ya serikali bila ya kukubali kuyumbishwa," alisema.

**ALICHOSEMA MBOWE**

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema haiwezekani kukitenganisha chama hicho na historia ya Hayati Lowassa kwa kuwa akiwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA alikuwa karama ya kuunganisha watu hasa vijana na kuwalea.

Alisema Lowassa alikuwa mwana demokrasia na alichangia sehemu kubwa ya chama hicho kupata viti 115 vya ubunge na madiwani zaidi ya 2,000 wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015.

"Wakati akiwa Mjumbe wa Kamati Kuu CHADEMA alikuwa ni mtu mnyenyekevu anayependa kusikiliza na kuonyesha njia, kadhalika alikuwa kiunganishi na kipenzi cha watu wengi kwa kuwa hakuwa mbaguzi," alisema Mbowe. Akizungumza kwa niaba ya familia, mtoto wa Hayati Lowassa, Fredrick Lowassa, alisema maisha ya baba yao yalikuwa tunu na nyota iliyong'aa ndani ya CCM na alipokuwa mtendaji na mtumishi serikalini.

"Itakuwa ni mtihani mkubwa kwa familia yetu kuvaa viatu vyake kutokana na hekima aliyokuwa nayo pamoja na uhodari wake. Ila tunashukuru Mungu kwa zawadi yake kipindi chote alichoumwa hadi mauti yalipomfika,"alisema Fredrick.

**MAJALIWA**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema baada ya msiba huo kutokea Rais Samia alitoa maelekezo ya kwa Kamati ya Maafa Kitaifa kuhakikisha kuwa wanafanya maandalizi vizuri ya msiba ili Hayati Lowassa azikwe kwa heshima.

"Naipongeza kamati kwa usimamizi wa kazi hii wamefanya kazi nzuri kwa kuwa shughuli imekwenda vizuri mpaka tulipotamatisha leo (jana), pia niwashukuru wananchi wote kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini kwa kujitokeza kwa siku tano kwenye maombolezo ya kuaga mwili wa mpendwa wetu," alisema.

# Wasiojulikana wadaiwa kubaka, kumuua mtu kwa kumnyonga

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana ambao wanatuhumiwa kumbaka, kumuua kwa kumnyonga Martha Zacharia (40), kisha mwili wake kuutupa pembezoni mwa barabara.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi (ACP) Mayila Mashenene, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa Februari 14, mwaka huu, katika Mtaa wa Makutano, Manispaa ya Sumbawanga huku akibainisha kuwa uchunguzi wa tukio hilo bado unaendelea.

Alisema Zacharia alikuwa mwimbaji wa kwaya ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Epiphania, Jimbo la Katoliki Sumbawanga na inadaiwa kuwa kabla ya kuuawa, alitoka kanisani kusali misa ya Jumatano ya Majivu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Isaya Lusambo, ambaye marehemu ni mama yake mdogo, alisema kabla ya kifo hicho Martha alikwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sumbawanga kumpelekea chakula mgonjwa na baada ya kutoka hapo, aliwaaga kuwa anakwenda kanisani.

Lusambo alisema baada ya kuondoka hakuwasiliana naye tena mpaka alipopigiwa simu siku iliyofuata na kujulishwa kuwa mama yake mdogo ameuawa na mwili wake umetupwa pembeni mwa barabara.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Makutano, Geoffrey Kangunga, alisema katika mtaa huo kumekua na matukio mengi ya watu kukutwa wamefariki barabarani, ambapo mpaka sasa yamefikia manne.

Alisema pia kumekuwa na matukio ya watu kubakwa na kuumizwa huku wengine wakiporwa pesa na vitu vingine walivyo navyo.

Kangunga alisema changamoto kubwa iliyopo ni kuwa maeneo ya pembezoni mwa Barabara ya Sumbawanga - Mpanda hayajajengwa nyumba, hivyo nyakati za usiku kunakuwa na giza hali inayosababisha watu wenye nia mbaya kujificha na kutekeleza vitendo vya kiuhalifu.

"Tunaiomba serikali igawe viwanja maeneo yaliyopo nje ya hifadhi ya barabara ili wajenge hali itakayosababisha kuwa na watu wanaoishi maeneo hayo, kwenye nyumba zao kutakua na taa za nje zitakazo saidia watu waovu kuacha kujificha katika maeneo hayo" alisema.

Mkazi wa mtaa huo, Lucy Moshi, alisema aliwahi kukabwa mpaka akapoteza fahamu, akapewa msaada na majirani zake ambao walimpeleka hospitalini na ndipo alipopewa huduma na kupata nafuu.

Alisema licha ya kwamba wamekuwa wakitoa taarifa kwa serikali ya mtaa lakini hakuna hatua yoyote inayochukuliwa.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa (RCO) wa Rukwa, Chacha Maro, alisema Zacharia ameacha mume na watoto wanne.

Pia aliwataka wakazi wa mtaa huo kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili watuhumiwa wa vitendo hivyo wakamatwe na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.




Mjane Mama Regina Lowassa na familia yake akisali mbele ya jeneza lenye mwili wa mumewe, Hayati Edward Ngoyai Lowassa nyumbani kwake, Monduli mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Katibu Mkuu CWT matatani madai ya vurugu mkutanoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Japhet Maganga, na wenzake 10 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kufanya fujo kwenye mkutano wa Baraza Kuu la chama hicho wakati wakipitisha bajeti ya mwaka.

Tukio hilo lilitokea juzi jijini hapa baada ya baraza hilo kuazimia kumsimamisha kazi Maganga kutokana na kupoteza sifa baada ya kufukuzwa kazi na mwajiri wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, amethibitisha kukumatwa kwa kiongozi huyo pamoja na wenzake wakati wa mkutano huo.

"Tulipata taarifa kuwa kuna watu wanafanya fujo tukaenda kudhibiti kabla hayajatokea madhara. Kwenye mkutano huo sisi hatufahamu ilikuwaje zikatokea fujo. Ukitaka kufahamu zaidi waulizwe CWT wenyewe," alisema Kamanda Otieno.

Kamanda Otieno alisema hadi jana mchana Maganga na wenzake 10 walikuwa bado wanashikiliwa na Jeshi la Polisi wakati wakisubiri hatua zingine za kisheria kuendelea.

Hata hivyo, taarifa ambazo Nipashe imezipata kutoka kwa mmoja wa wajumbe wa CWT waliokuwamo katika mkutano huo (jina limehifadhiwa) ni kwamba baada ya baraza hilo kuazimia kwa kauli moja kumsimamisha kazi Maganga, ndipo zilipozuka fujo hali ambayo ilisababisha Polisi kuingilia kati na kumkamata yeye na wenzake 10.

Rais wa CWT, Leah Ulaya, akizungumza na waandishi wa Habari, alisema baraza liliazimia kwa kauli moja kumsimamisha kazi Maganga kutokana na kupoteza sifa ya kukiongoza chama hicho.

"Sababu za kumsimamisha kazi ni kwamba alifukuzwa kazi lakini pia Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi nchini aliandika barua kwa kiongozi mkuu wa CWT yaani Rais wa chama, ndipo baraza kuu lilipoazimia kuwa aondoke," alisema.

"Iliazimiwa aondoke kwa sababu hana sifa hiyo, ndiyo sababu iliyofanya zitokee vurugu kidogo hadi Jeshi la Polisi kuingilia kati. Lakini ukiondoa hilo, hivi sasa mkutano wetu unaendelea vizuri," alisema Ulaya.

Baadhi wa wajumbe wa baraza hilo wakizungumzia sakata hilo, wako walioungа mkono uamuzi wa kusimamishwa kazi kwa Maganga na wengine kupinga kwa madai kuwa ni kinyume cha katiba ya chama na kanuni zake.

Mwakilishi wa wenyeviti wa CWT kwenye baraza hilo, Emmanuel Kiheko, alisema kuna mahali wamekosea katika kumwondoa Maganga.

"Endapo tunadhamiria kumwondoa Maganga wakati katiba na kanuni hazitupi nguvu hizo, tunaelekea kubaya. (Hezekiah) Oluoch (aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CWT) tulimlipa zaidi ya Sh. milioni 300 sasa sijajua Maganga tutamlipa kiasi gani," alisema.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 107 of 2023**
**In the Matter of the Estate of the LATE**
**GAUDENCIA BENEDICT MAGAGA**
**Of Kikuyu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by**
**THERESIA LAWRENCE MAGAGA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 11 day of 10......................... 2023

Dated at Dodoma this 20 day of 09..............2023

**RESIDENT MAGISTRATE**

**TAARIFA KWA UMMA**

SISI KAMPUNI YA USAFIRISHAJI YA GLENRICH TRANSPORTATION CO. LTD, TUTASAFIRISHA MZIGO MPANA KUTOKA KURASINI KWENDA KIWALANI SIKU YA TAREHE 18/02/2024, NJIA TUTAKAYOTUMIA NI BARABARA YA MANDELA KUPITA BARABARA YA PUGU, MAGARI YATAKAYOTUMIKA NI HAYA YAFUATAYO:-

- **T483 DAU/T483 BXU**
- **T969 DLD/ T 293 DDA**
- **T 214 DCB/ T 866 DRK**
- **T 710 CRR/ T 870 DRK**

UPANA WA MZIGO NI MITA 4.3.

WAKO KATIKA UJENZI WA TAIFA.

TRANSPORT MANAGER
GLENRICH TRANSPORTATION CO. LTD

# Simulizi Askofu aliyewasema viongozi wa serikali bila woga

Na Mwandishi Wetu

KATIKA sehemu ya kwanza ya simulizi za Askofu Dk. Zephaniah Kameeta (pichani), ilielezwa kuwa ni mtu mwenye ualbino, kasisi na askofu, mfungwa wa kisiasa, mwanasiasa na mpigania uhuru na haki za binadamu.

Dk. Kameeta (79), raia wa Namibia ambaye kutokana na historia yake, amejijengea umaarufu tangu akiwa kijana. Ni kiongozi wa kiroho, kisiasa na kijamii aliyejipambanua kujali zaidi jamii kuliko maisha yake na ya familia yake kwa ujumla.

Aidha, ilibainishwa kwamba wakati wa harakati za ukombozi wa Namibia, Dk. Kameeta, ambaye kwa sasa ni Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Jamhuri ya Namibia (ELCRN), alikuwa mstari wa mbele kupambana na udhalimu na unyanyasaji. Hakujali kuhatarisha maisha yake na hata katika hotuba zake kwenye makongamano na mikusanyiko mbalimbali alikuwa mstari wa mbele kuhamasisha Namibia na Afrika Kusini kuwa huru dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi.

Harakati zake hizo zilisababisha kukamatwa, kuwekwa kizuizini na hata kufungwa. Pia kutokana na kupinga kwake waziwazi ubaguzi wa rangi na aina mbalimbali za ukandamizaji, mara kadhaa aliwahi kunyang'anywa hati yake ya kusafiria na serikali ya Afrika Kusini, wakati wa utawala wa makaburu.

Kuwekwa kizuizini na kufungwa hakukumfanya arudi nyuma katika yale aliyoyaamini na kuyasimamia. Alisema wazi hata mbele ya viongozi wa serikali walivyokwenda kinyume. Kwa kufanya hivyo, alijipambanua kuwa ni mtu muwazi na asiyependa kupindisha mambo.



### ZABURI KWA UKOMBOZI

Kutokana na nafasi yake na kutambulika kama mwanatheolojia ya ukombozi (Liberation Theology). Dk. Kameeta alitumia Zaburi kama mwongozo wake kwenye mapambano na aliigeuza na kutumia maneno yake ambayo kwa tafsiri isiyo rasmi yanasema: "Bwana ndiye mchungaji wangu; ninacho kila ninachokihitaji. Ananiongoza katika kuiona nchi ya haki na amani na ananiongoza katika hatua zangu kwenye nchi hii.

"Ananitia nguvu. Ananiongoza katika njia ya ushindi, kwa kuwa ameniahidi. Hata vurugu za hali ya juu zikitokea sitaogopa. Kwa kuwa Bwana uko pamoja nami. Nguvu yako na pendo vyanilinda. Unaniandaa kwa ajili ya uhuru wangu.

"Adui zangu wanaponiona, unaniita kuwa mgeni wa heshima. Umekijaza kikombe changu haki na amani. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; na upendo wako wa ukombozi utakuwa makazi yangu."

### WAJIBU WA KANISA

Askofu Kameeta katika maisha yake ya utumishi, alilikumbusha kanisa umuhimu wa kuisaidia jamii. Tangu mwaka 1971 aliweka wazi kuwa kanisa haliwezi kujitenga na jamii kulingana na hali halisi ya wakati uliopo.

Wakati huo, pamoja na kuwa mchungaji na mwalimu wa theolojia, alikuwa akihimiza umuhimu wa watu kuwa huru na kupata haki bila ubaguzi. Alikuwa mstari wa mbele kuzungumzia haki na maridhiano ndani ya Namibia bila kujali hali ya kisiasa iliyokuwapo ndani ya nchi hiyo na Afrika Kusini chini ya ubaguzi wa rangi na utawala wa mabavu.

Kuhusu wajibu wa kanisa katika mapambano dhidi ya Ukimwi, alisema halipaswi kusita kusema kuhusu janga hilo ambalo dunia haizungumzi kwa wazi na kwa kina huku wanaoathirika wakiwa waumini wao.

Mbali na Ukimwi, alisema jamii haiwezi kuwa huru ikiwa kuna mtoto ndani ya Namibia anayepoteza maisha kwa sababu ya njaa na utapiamlo. Alisisitiza kuwa nchi haiwezi kusema iko huru wakati kuna mamilioni ya watu wanapata shida, wakiwamo watoto ambao wanasumbuliwa na maradhi.

### KUWAONYA VIONGOZI

Kameeta pia alikuwa akiwaonya viongozi ambao wanapewa nafasi ya kuwatumikia wananchi lakini hawafanyi hivyo, badala yake wanatumia nafasi hizo kujinufaisha. Aliweka bayana kwamba baadhi ya watu baada ya kushinda katika uchaguzi na kupewa nafasi za juu za uongozi, wanabadilika kutoka watu wa kawaida na kujiona miungu watu.

"Jambo hilo lisiwafanye watu kuwa mashuhuri au wa hali ya juu. Watu wanaoingia katika tabia hizo wanajiweka katika mazingira mabaya kwa mustakabali wao. Hali hiyo inatengeneza anguko la mtu. Tuwe kama tulivyokuwa kama tulivyokuwa kabla ya kupata nafasi za uongozi.

Jambo la muhimu kwangu baada ya kupata nafasi katika uongozi ni kwamba uhusiano wangu na watu unabaki kama awali siwezi kumdharau mtu yeyote, hata mfagizi mtaani. Hili ndilo la muhimu kwa viongozi.

Dk. Kameeta alihimiza viongozi wanapochaguliwa watambue kwamba wana mzigo mkubwa katika kuwahudumia wananchi na si kujikweza na kutumia nafasi zao kwa maslahi binafsi. Aliwataka viongozi kushirikiana na wananchi kutokomeza umaskini na kuhakikisha rasilimali zinagawanywa kwa usawa bila kujali hali ya mtu.

Katika moja ya hotuba zake, kiongozi huyo wa kiroho ambaye pia aliwahi kuwa Naibu Spika wa Bunge la Namibia na Waziri wa Kuondoa Umaskini na Ustawi wa Jamii, aliwahi kusema wananchi wanapaswa kushirikishwa katika masuala yanayowahusu yakiwamo ya demokrasia.

Alisema ili demokrasia istawi katika jamii, elimu na ushiriki wa wananchi ni mambo muhimu na ndiyo msingi wa haki, amani na maendeleo kwa raia wote bila ubaguzi wa aina yoyote.

"Maendeleo ya ustawi haviwezi kufikiwa katika mazingira ya kutokuaminiana, utengano, hofu na uhasama. Kama tunataka maendeleo ya kweli, hatuna budi kuondokana na vikwazo hivi na hapo ndipo amani na ustawi vitapatikana," alisema wakati wa uzinduzi wa Dira ya Maendeleo ya Namibia ya mwaka 2030.

### KIMATAIFA

Kutonana na kuwapo katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa, Askofu Kameeta hakusita kuonyesha sura yake halisi katika masuala mbalimbali yanayohusu jamii. Mwaka 2003 akiwa makamu wa Rais wa Fungamano la makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) Kanda ya Afrika, alipinga matumizi ya nguvu katika kusuluhisha migogoro katika baadhi ya mataifa.

"Tukiwa watu tulioitwa kuhubiri haki na amani, tunakataa matumizi ya nguvu na tunasikitika matumizi hayo," alisema Dk. Kameeta katika kikao cha maandalizi mkutano wa LWF Kanda ya Afrika mwaka 2003, Nairobi nchini kenya.

Alisisitiza kuwa mataifa mengi ya Afrika ambayo kanisa hilo lina waumini, yameathiriwa na vita kwa kiasi kikubwa, hivyo matumizi ya nguvu yanawarejesha watu katika machungu waliyopitia. Aliyataka makanisa katika mataifa hayo kuhubiri amani na pale penye migogoro mazungumzo yachukue nafasi na si matumizi ya nguvu.

Kameeta aliyataka makanisa ya Kilutheri kujitoa na kushiriki katika masuala ya watu wenye uhitaji wakiwamo wafungwa, waliosetwa na kukumbwa na madhila mbalimbali na wanaoishi na virusi vya Ukimwi.

Kama tutakuwa tunasikia tu na kuzungumza bila kuchukua hatua tutakuwa wasaliti wakubwa wa dunia," alisema.

Sambamba na kuhubiri amani, aliyahimiza mataifa ya Afrika kuwa sehemu ya uwajibikaji katika matatizo yanayolikabili bara hilo huku akionya mtindo uliotawala wa kuyalaumu mataifa yaliyotawala Afrika wakati wa ukoloni.

"Tunahitaji ushirikiano mpya kwa mabadiliko Afrika," alisema Kameeta akirejea Mpango wa Ushirikiano Mpya wa maendeleo Afrika (NEPAD), mpango ulioasisiwa na viongozi wa serikali za Afrika wakihimiza sera za uwazi na Uchumi imara ili kuiwezesha Afrika kushiriki katika Uchumi wa dunia.

HABARI KITAIFA

# Kituo mafunzo ya afya chazinduliwa

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya huduma za Afya ya Aga Khan Tanzania (AKHST) chini ya ufadhili wa mradi wa Kuboresha Huduma ya Dharura Nchini (IMECT), imefungua kituo cha mafunzo ya dharura cha kisasa na kutoa vifaa katika vituo saba vya afya vyenye thamani ya Sh. milioni 641.3

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya kuzinduliwa kwa kituo hicho kilichogharimu Sh milioni 182, Mratibu wa Mradi huo, Dk. Hussein Manji, alisema: "Tumeamua kuanzisha kituo hiki kwa sababu bado kuna changamoto katika kutibu magonjwa ya dharura."

Manji ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya dharura, alisema kituo hicho kitafanya kazi na vituo vya afya vya serikali na binafsi lengo ni kuhakikisha kunakuwa na huduma bora za dharura kwa wananchi.

Dk. Manji alisema hatua hiyo kubwa ya maendeleo imefanikiwa kwa ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsiuliofadhiliwa na serikali ya Poland, Huduma za Afya za Aga Khan Tanzania kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania.

"Tangu kuzinduliwa kwa mradi huo Septemba 2022, mradi wa IMECT umeonyesha uwezo wa ushirikiano wa Kimataifa na ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika kushughulikia mahitaji muhimu ya afya," alisema Dk. Manji.

Alisema vituo saba vya kutolea huduma za dharura ilivyopatiwa msaada wa vifaa ni hospitali za rufani za Mwananyamala na Temeke, Hospitali ya Wilaya ya Chanika, Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza, Tanzania Poland Emergency Medical Training Center, Aga Khan Hospital Dar es Salaam (AKHD), Aga Khan Polyclinic Old Dispensary Zanzibar na Vituo vingine vya afya.

Alisema mchango huo mkubwa unasisitiza dhamira ya wadau wote katika kuboresha ubora na upatikanaji wa huduma za dharura.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Gunini Kamba, alisema uzinduzi wa kituo hicho cha mafunzo na makabidhiano ya vifaa muhimu vya matibabu ni hatua kubwa katika juhudi za serikali za kuimarisha huduma za matibabu ya dharura nchini.

"Tunashukuru kwa msaada wa serikali ya Poland, Kituo cha misaada cha kimataifa cha Poland, Huduma za Afya za Aga Khan Tanzania na washirika wetu wote katika mradi huu ambao utaenda kusaidia uboreshaji wa huduma za dharura," alisema.

# Biashara nyama ya punda yafanywa kificho

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

LICHA ya serikali kuvifunga viwanda viwili vya kuchinja nyama ya punda katika mikoa ya Shinyanga na Dodoma, imebainika biashara ya mnyama huyo bado inaendelea kufanyika kinyemela.

Hatua hiyo inatishia kuhatarisha kutoweka kwa mnyama huyo endapo hatua za kusitisha hazitachukuliwa.

Hayo yamebainika juzi wakati wa mafunzo ya siku mbili ya waandishi wa habari kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Shinyanga yaliyoandaliwa na Shirika la IFTz, linalojihusisha na maendeleo ya wakulima, Uchumi na ustawi wa jamii.

Mkuu wa programu kutoka shirika hilo, Jacqueline Nicodemus, alisema pamoja na serikali kuvifunga viwanda vya nyama ya punda na kupiga marufuku biashara ya nyama, ngozi na uchinjaji lakini bado biashara hiyo inaendelea kufanyika kinyemela.

Alisema shirika la IFTz kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine bado linaendelea kukabiliana na kudhibiti vitendo vya kuchinja punda.

Alisema mwaka 2021 baada ya kufungwa kwa viwanda vya kuchinja nyama ya punda ambavyo ni Fang Hua kilichokuwa Kijiji cha Ibadakuki Manispaa ya Shinyanga na Huwa Cheng kilichokuwa Dodoma, kulifanyika mkutano jijini Dar es Salaam na kutoa maazimio kadhaa mojawapo ni kumlinda mnyama huyo.

"Katika mkutano huo ilitolewa tamko ambalo liliwekwa msisitizo wa zuio la Serikali ya Tanzania kwamba hakutakuwa na biashara ya zao la punda hadi punda watakapifikia milioni 10 Tanzania," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Mbarwa Kivuyo, alisema wameanzisha kampeni ya kulinda punda na kuhakikisha wanapata haki za msingi za mnyama kwani kwa sensa iliyofanyika imeonyesha idadi ya punda nchini ni 600,000.

Alisema pamoja na kuwepo kwa sera na sheria na kufungwa kwa viwanda vya kuchinja nyama ya punda, lakini bado wanaendelea kuchinjwa.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema inapaswa serikali kuangalia namna ya kuhakikisha idadi ya punda inaongezeka mara kwa mara kama ilivyo kwa wanyama wengine.



Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, ofisini kwake Bungeni, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Pamoja na mambo mengine, Mshomba alimpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa IPU. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil.10/- kuwalinda wanafunzi wa kike

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

DOLA za Marekani 476,000 (zaidi ya Sh.bilioni 10) zinatarajiwa kutumia katika kuboresha mazingira ya kujifunzia, kuwalinda na kukuza maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana SEGA iliyoko Mkundi mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Shirika la SEGA, Laina Mwandoloma, alisema kupitia Shirika la Naturing Minds kutoka Marekani ambalo ndio mdhamini shule hiyo wamepata fedha hizo kutoka Shirika la USAID kupitia Idara ya Shule na Hospitali nje ya Marekani (ASHA).

Mwandoloma ambaye pia ni Meneja wa Shule hiyo, alisema fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa kuongeza miundombinu ya kisasa shuleni hapo ikiwemo bweni litakalobeba wasichana 48, maabara ya biolojia ambayo imekua ni hitaji la muda mrefu la shule hiyo, uzio wa shule, karakana na kibanda cha mlinzi.

Alisema ujenzi huo utaboresha mazingira ya kujifunzia na kuhakikisha usalama wa wanafunzi, huku ukiipa nafasi shule kuongeza na kuhudumia wanafunzi wengi zaidi.

Pia alisema ujenzi wa uzio wa shule utaimarisha usalama kwa wanafunzi, kwa sasa shule imezungukwa na makazi ya watu hivyo inahitaji mazingira yenye amani na utulivu ya kusoma ili kuzuia vishawishi kwa wanafunzi kutoka nje ya shule.

Mwandoloma alisema mradi huo pia utapanua wigo wa shule kwa kutoa mafunzo kwa vitendo ikiwemo katika muziki, ufugaji kuku, ushonaji na kilimo cha mboga, jambo ambalo linatarajiwa kuwa na manufaa kwa wanafunzi na jamii ya SEGA.

Kwa mujibu wa Mwandoloma. mradi huo unalenga kudumisha uhusiano wa kirafiki kati ya Tanzania na Marekani kwa kukuza misingi muhimu ya usawa wa kijinsia, uvumbuzi katika teknolojia na uvumbuzi katika mbinu za kufundishia na kujifunza.

Alisema mradi huo unajikita katika ujenzi endelevu unaolenga utunzaji wa mazingira na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mwandoloma alisema kwa sasa shule hiyo inahudumia wanafunzi 280 wenye ulemavu na wenye vipaji.

Alisema utekelezaji wa mradi huo umeshaanza kwa hatua za awali Oktoba, mwaka jana, na unatarajia kukamilika Septemba mwaka 2027.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Lowassa ameacha funzo kubwa kwa Watanzania, wajifunze sasa

**HATIMAYE** Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa, amemaliza safari ya maisha yake duniani, baada ya jana kuzikwa nyumbani kwake, Monduli mkoani Arusha. Lowassa alifariki dunia Jumamosi iliyopita katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Tangu kutokea kwa kifo chake, watu mbalimbali walizungumza mambo mazuri aliyoyafanya kwa taifa katika nafasi mbalimbali alizoshika katika serikali na utumishi wa umma, zikiwamo Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Miji, Waziri wa Maji na Mifugo, na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais.

Wanasiasa wakongwe na walioko madarakani pamoja na viongozi wa dini, walitoa kauli mbalimbali zinazomwelezea kuwa alikuwa mtu wa watu kutokana na kujali kwake watu wanyonge na kuwasaidia. Hakuwa mbaguzi wa imani kwa kuwa hata alipoalikwa kwenye hafla mbalimbali za kuchangia maendeleo ya taasisi za dini, alikubali na kutoa michango yake kwa uzito ule ule.

Ni kweli kwamba katika nafasi za uongozi alizoshika, Lowassa alionyesha uwezo wake wa hali ya juu ikiwa ni pamoja na kupanga, kusimamia kile alichokiamini kwamba kina manufaa na matokeo chanya yanayotarajiwa. Katika kuhakikisha anayoyapanga yanatekelezwa, kwa watendaji alikuwa akitumia maneno nataka, naagiza na tekeleza. Neno kwamba naomba kwake ulikuwa msamiati mgumu.

Katika sekta zote alizosimamia, matokeo yalionekana na alipokuwa Waziri Mkuu, kutokana na nafasi hiyo kuwa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za serikali, alizunguka kila sekta na kuhakikisha yale wanayokubaliana yanatekelezwa. Wale walioshindwa kuyatekeleza hakuwa na mswalie mtume nao, aliwaondoa bila kujali ni watu wa namna gani.

Watu walishuhudia jitihada zake katika maendeleo ya elimu ya sekondari baada ya kuanzishwa kwa shule za kata hasa baada ya wanafunzi kuongezeka huku miundombinu ikiwa haijakamilika. Alikutana na wakuu wa mikoa na kuagiza kuwa ndani ya muda mfupi waliojiwekea kazi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa iwe imekamilika. Hakuagiza tu bali aliwaambia ukweli kwamba atakayeshindwa kufanikisha hilo afungashe.

Kwa jumla Lowassa alikuwa mtu wa kuthubutu kutokana na kiu yake ya kutaka mambo yafanikiwe. Hata taifa lilipoingia katika mgawo wa umeme, alitafuta suluhu ya kutafuta kampuni za kufua umeme ili nchi isiwe gizani. Yaliyotokea kuhusu Richmond ni historia lakini alionyesha moyo wa kuthubutu ili kuhakikisha nchi inapata nishati hiyo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Lowassa pia alikuwa mvumilivu na mtu wa kupenda amani. Hilo lilijidhihirisha mwaka 2015 baada ya matokeo ya urais yaliyompa John Magufuli (naye sasa marehemu) ushindi wa urais. Kulikuwa na madai kwamba Lowassa alikuwa ameshinda uchaguzi huo na wafuasi wake walitaka kupinga lakini aliwaambia wamwachie Mungu.


Alama nyingine kubwa ambayo Lowassa ameiacha ni maendeleo katika jimbo la Monduli aliloliongoza kwa takriban miaka 20. Kama zilivyo sehemu nyingi kame kwenye ukanda wa Umasaini, Monduli nayo ni mojawapo lakini alipambana kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Pia alipambana kuhakikisha Watoto wa jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai wanapata elimu na shule nyingi zilijengwa, si Monduli tu bali maeneo mengi ndiyo maana watu wa jamii hiyo walimlilia baada ya kusikia amefariki dunia.

Kutokana na sifa hizo, Lowassa ameacha fumbo kubwa na elimu kwa viongozi kuwa wanapaswa kutanguliza maslahi ya umma na si binafsi. Ni wazi kwamba kama kila kiongozi anayepewa dhamana ama kwa kuchaguliwa au kuteuliwa katika nafasi fulani atatekeleza wajibu wake ipasavyo, hakika Tanzania itaupiga teke umaskini. Lowassa ameacha funzo kubwa kwa viongozi na Watanzania kwa ujumla. Tujifunze kutoka kwake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

## Programu hii Taasisi ya Ustawi wa Jamii imekuja wakati sahihi



Na Sabato Kasika

**TAASISI** ya Ustawi wa Jamii, imeanza kuendesha programu mbalimbali ikiwamo inayolenga kutatua matatizo yanayoikabili jamii, hasa malezi na makuzi ya watoto na vijana baada ya kuona kuwa kuna hitaji hilo.

Hayo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Joyce Nyoni, katika taarifa yake ambayo gazeti hili limepata nakala yake akielezea maendeleo ya chuo, ambacho hivi karibuni kilitimiza miaka 50.

Yako mengi ambayo Dk. Nyoni anaelezea kwamba wamekuwa wakiboresha mitaala yao mara kwa mara, na kwamba sasa wameanza programu ya malezi na makuzi ya watoto baada ya kuona kuna hitaji kubwa la malezi na makuzi ya watoto na hasa vijana.

Ninaweza kusema kuwa programu hii ya Chuo cha Ustawi wa Jamii, imekuja wakati sahihi, kutokana na ukweli kwamba matukio mengi ambayo yamekuwa yakitokea ndani ya jamii, mengi yanasababisha ukosefu wa malezi bora na makuzi kwa watoto na vijana.

Matukio ya ukatili wa kila aina ukiwamo ulawiti, ubakaji, mauaji na mambo mengine yanayofanana nayo, ninaamini kuwa chanzo chake ni ukosefu wa elimu ya malezi bora na makuzi ndani ya jamii.

Kama anavyoeleza mkuu wa chuo, kuwa kutokana na mahitaji hayo, wameamua kujikita katika kuandaa wataalamu watakaokuwa sehemu muhimu ya makuzi na malezi ya watoto na vijana, hilo ni jambo jema. Si siri kwamba ndani ya jamii kuna mmomonyo mkubwa wa maadili, hivyo bila kuwapo jitihada mbalimbali za kunusru kizazi kijacho, taifa la baadaye linaweza kuwa la watu wa ajabu.

Kwa kuwa chuo hicho, kinaandaa programu ya saikolojia ili kusaidia watu kupata uhitaji wa wataalamu hao, ni wazi hatua hiyo itakuwa na manufaa makubwa iwapo itazingatiwa na jamii.

Utaratibu huo wa ushirikishwaji wa jamii kwa kuchangamana nayo ili kujifunza na kufanya kazi nayo na uanagenzi, kutakuwa na mchango mkubwa wa wahitimu kupata nafasi ya kuunganisha nadharia ya darasani na uhalisia kwenye jamii.

Hivyo, kwa njia hiyo, jamii itaweza kusaidiwa kurudi kwenye mstari na kuzingatia malezi na malezi ambayo hayaendi kinyume na mila na desturi za Kitanzania ambazo zimeanza kuharibiwa.

Kimsingi, kuvunjika kwa maadili katika familia na jamii kwa ujumla ni mojawapo ya sababu zinazotajwa kuchangia kwa viwango vikubwa kutokea kwa wimbi la vitendo vya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji.

Uporomokaji wa maadili miongoni mwa jamii wa Kitanzania, imeleta athari zinazochangia kutokea kwa viwango vikubwa vya wimbi la vitendo vya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji.

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya watu wazima na vijana kusambaza picha za ngono kupitia mitandao ya kijamii ambazo wakati mwingine zinatazamwa na watoto wadogo.

Kwa kuwa chuo hicho kimeamua kutojikita katika taaluma ya darasani tu na kwenda kufanya kazi ndani ya jamii, ninadhani ni vyema programu hii iungwa mkono ili ilete matokeo chanya.

Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, wawe tayari kushirikiana na wataalam kutoka chuo hicho, ili kile ambacho kimekusudiwa kufanywa kiweze kuwafikia walengwa wote ili kuokoa kizazi kijacho.

Inawezekana wazazi, walezi wameshindwa kuchukua hatua za kusimamia malezi mema na kusabisha watoto wao wajiingize katika vitendo vya mmomonyoko wa maadili.

Lakini kupitia programu ya Taasisi ya Ustawi ya Jami, inawezekana kuwa na mabadiliko makubwa ya kurudisha jamii kwenye mstari iwapo jamii itaipa programu hiyo uzito wa kutosha.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Pumzika kwa amani Lowassa, kazi umekamilisha, mwendo umeumaliza



Pascal Mayalla

TANGU kumetokea msiba wa Edward Lowassa, kule Jamiiforums tukimwita kwa jina maarufu la Mwamba wa Kaskazini, Jumamosi iliyopita, Jana alipopumzishwa kwenye makao yake ya milele. Sikufanikiwa kuandika kitu chochote kumhusu Mwamba huyu na baada ya kupumzishwa, sasa ndiyo angalau nimeweza kutulia na kuandika kitu.

Kwa mazingira ya kazi yangu ya uandishi wa habari, nikihudumu kwenye vyumba vya habari toka mwaka 1990 hadi 2020 na Lowassa akiwa kiongozi, hakuna mwandishi yoyote wa habari ambaye hakuwahi kukutana na Lowassa. Binafsi katika kipindi chote hicho, nimekuwa nikimwandika kwenye kazi mbalimbali za kihabari.

Siku zote na dunia nzima, habari ni bure, hivyo sisi waandishi wa zamani, zaidi ya mishahara kwenye kazi zetu, tulikuwa tunaandika habari bure. Japo mpaka sasa habari bado ni bure, kuna habari lazima utumie gharama kuzipata ili uziandike.

Lowassa akiwa Waziri wa Maji na Mifugo, nikapangiwa kuzunguka naye kwenye ziara ya kutembelea ranchi za taifa. Tulilipwa fedha za kujikimu na ofisi lakini wizara ilitoa usafiri. Waandishi tukahesabiwa tuko wangapi, kwa kawaida waandishi huwa hatupangiwi gari maalum bali tunabananishwa katika magari yoyote ya kwenye 'pool' na muda mwingi huwa ni magari mikweche na tunakuwa wa mwisho kufika kwenye tukio.

Hata hivyo, kwenye ziara za Lowassa, waandishi tumetengewa gari maalum na si mikweche! Gari la waandishi lilikuwa moja ya magari ya mwanzo kwenye msafara na si mwisho kama ilivyozoeleka. Kila tunapokwenda tunakuta tumeshatafutiwa mahali pa kulala hoteli nzuri wanazofikia viongozi, hivyo atakapofikia yeye ndipo waandishi mtafikia na zimelipiwa.

Kwa hiyo posho uliyopewa unakunja na kuiweka kibindoni.

Kama hiyo haitoshi, kila jioni unasainishwa bahasha nyingine yenye posho nene, hivyo kwangu ziara za Lowassa ndizo zilizonifungulia mishiko ya waandishi au bahasha za waandishi.

Toka wakati huo, Lowassa akaagiza kwenye mikutano, semina, warsha, makongamano na ziara za viongozi, kama mnalipana posho, waandishi wa habari nao pia ni binadamu, hivyo nao wanastahi kulipwa posho.

Hapo ndipo bahasha rasmi za waandishi zikaasisiwa na kurasimishwa. Siku hizi kuna baadhi ya habari bila kuwaangalia waandishi kwa hizi bahasha za posho, hawatoi kitu na imefikia hatua baadhi ya waandishi kuwa wawazi kama tukio halina posho, usinialike!

Pia akiwa kwenye wizara hiyo yenye sekta za maji na mifugo, kulianzishwa wiki ya maji ambayo mwenyewe aliiasisi.

Waandishi wanaoalikwa kushiriki barua zao ziliandikwa wajigharimie usafiri, watarejeshewa fedha zao. Mwaliko ule nikampanga Mhariri nipangiwe mimi.

Siku zilipokaribia nikaulizia vipi hii tripu, nikaelezwa kumetokea kazi nyingine nyingi muhimu zaidi, hivyo sisi TBC hatuna mtu wa kamera kwenda kuripoti tukio hilo, nikamwambia mhariri mimi nina kamera yangu na nitaripoti mwenyewe, nikapewa ruhusa.

Hapa si kwamba najidai, bali mimi ndiye mwandishi wa habari wa kwanza wa Tanzania kufanya kitu kinaitwa VJ (Video Journalist).

Vyombo vyote vya habari vinatumia watu wawili, mmoja ni mwandishi wa habari ni mwingine ni mpigapicha. Mimi licha ya kuwa ni mwandishi wa habari pia nilikuwa ni mpigapicha, hivyo ikitokea upungufu wa wapigapicha, naandika habari mwenyewe, napiga picha mwenyewe.

Nikifika chumba cha habari nafanya kila kitu mwenyewe na kuhariri kisha naingia studio kuisoma.

Hivyo Wiki ya Maji nikabeba kamera yangu nikasafiri kwa gharama zangu. Ilikuwa Arusha, japo nilitumia usafiri wa basi, kule nikajiongeza kwa kujisajili tuko wawili na tumetumia usafiri wa ndege, ili kurudishiwa nauli nene.

Kazi ya kwanza ni kumtafuta mtu wa kujifanya ndiye mpigapicha wangu, nikampata nikampiga picha na kumsajili kama mpigapicha wa TBC. Wakati wa kutia saini posho, si wale jamaa wa malipo wakaomba kila mtu aonyeshe kitambulisho cha ofisi, nikajiuliza sasa itakuwaje?, lakini mambo yote yalifanikiwa na posho kama ilivyo kwa watu wawili ikafanikiwa kutolewa.

Nilirudi ofisi, nikaandika habari yangu na kuwatengenezea kipindi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa safari za Mzee Lowassa.

Nini mengine Lowassa aliyafanya? Tukutane wiki ijayo kwa sehemu ya pili ya Buriani ya Lowassa upate kisa jinsi Edward Lowassa alivyookoa maisha ya Mtanzania mmoja huko Rome, Italia.

Pumzika Lowassa Pumzika, Kazi Umekamilisha, Mwendo Umeumaliza, Pumzika!

**Paskali**
**255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Sura mbili za Watanzania msiba wa Lowassa



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KWENYE familia yoyote ndugu hawakosi kusigana katika baadhi ya mambo, na kuna nyakati hufikia hata kupigana na kutengana kabisa tena ndugu wa damu na kuiacha na sintofahamu.

Kuna nyakati hutokea ndugu mmoja katika familia, akawa anasemwa vibaya na ndugu zake wakati hayupo, lakini akiwapo huonekana kumchekea na kuonekana mmoja wao, lakini wakimchukia kimoyomoyo.

Sababu za kuchukiana hutofautiana kati ya ndugu na ndugu, na wakati mwingine unafiki hutawala miongoni mwao, kwa kuwapo wanaojikomba kwa ndugu mmoja kwa kutarajia maslahi fulani.

Watu wa aina hiyo huwa ni wabaya, kwani hukuchekea jino pembe ukiwapo na ukiondoka wanaongoza kukung'ong'a na kukuponda kana kwamba huwajawahi kuwa ndugu miongoni mwao.

Jana alilazwa mahali pema peponi, Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, huku kifo chake kikinikumbusha aina hii ya maisha baada ya kuona jinsi alivyoishi akipitia vipindi vya raha na karaha, mpaka alipoaga dunia Februari 10, mwaka huu.

Kwa mtu ambaye hakupata kumfahamu Lowassa na alichokifanya enzi za uhai wake, simulizi zilizotolewa wakati wa msiba wake, zingetosha kutoa picha kamili ya alikuwa mtu wa aina gani.

Kama hukuwa mfuatiliaji wa maisha ya kiongozi huyo, bila shaka simulizi hizo zitakwambia kuwa alikuwa kiongozi imara na mwenye msimamo imara ambaye hakutakiwa kuaga dunia katika siku hizi.

Lakini kwa waliomfahamu Lowassa tangu miaka hiyo ya siasa hususan akiwa Tanganyika African National Union (TANU), Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wanaweza wakaja na picha tofauti ya milima na mabonde katika maisha yake.

Lowassa ni kiongozi aliyetukanwa na kubezwa sana akipitia maisha magumu sana akiwa CHADEMA mpaka kurejea CCM. Akiwa CCM awali aliishi katika familia iliyokuwa ikimchekea na kumsifia, hata kujisikia kutosha kuwania urais na kukubalika.

Alipokosa nafasi hiyo kwa alichokichukulia kuwa ni uonevu akiungwa mkono na baadhi ya watu wake wa karibu, alihamia CHADEMA, ambako alimwagiwa matusi, kejeli za kila aina na kuonekana mtu asiyekubaliwa.

Waliosalia ndani ya familia yake baada ya yeye kujitoa, ndio walioongoza kumtukana, kumkejeli na kumchafua kwa majina mbalimbali huku wakitweza utu wake na baadhi kumtabiria kuwa Rais atakayefia Ikulu endapo angechaguliwa.

Wako waliosema alikuwa nyuma ya watu waliokuwa wakiisumbua CCM, akiwatuma na akiwapa fedha ili kuibomoa kwa utajiri wake ambaye kwa mujibu wa ndugu zake hao, hastahili kuwa karibu na masikini kwa kuwa ni tajiri hivyo asingeweza kuongoza Watanzania masikini.

Waliokuwa wakimtukana na kumbeza Lowassa kipindi cha kampeni za mwaka 2015 akiwania urais kwa tiketi ya CHADEMA wakisema ni mgonjwa anayejichafua majukwaani, hivyo kutofaa kuishi Ikulu kutokana na afya yake, ndio waliojitokeza kumlilia msibani.

Msiba huu ulikuwa kama fumbo kwa baadhi ya watu waliojitokeza kula matapishi yao, kana kwamba hawakuwa wakijulikana kimisimamo dhidi ya Lowassa na sasa kumonesha walikuwa karibu naye muda wote kumbe unafiki mtupu.

Ruge Mutahaba (ssa marehemu) alipata kusema, cheza na kingine lakini si Mungu na Teknolojia. Safari hii teknolojia ikaumbua baadhi ya wanasiasa hususan wa CCM, waliokuwa mahasidi kwa Lowassa na kujitokeza kutaka kufuta makosa yao wakati wa msiba.

Ni bahati mbaya sana, kwamba walichokuwa wanakifanya kilionekana dhahiri, kwa waliokuwa wanawajua na hata Lowassa mwenyewe hakutaka jeneza lake lifunuliwe ili wamwone na kumbeza akiwa kwenye umauti.

Ingawa sina uhakika, lakini inawezekana kabla hajaaga dunia, aliita familia yake na kuitaka kamwe isifunue jeneza lake wakati wa heshima za mwisho, akijua kuwa siku hiyo mahasimu wake wangekwenda kumtazama kwa jicho la kejeli.

Yawezekana Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanznaia (KKKT), Dk. Alex Malasusa, alikuwa sawa kusema kufunua jeneza wakati wa kuaga si lazima ila ni hiari, lakini kwa mtu kama Lowassa ilikuwapo haja ya kufunuliwa ili kila mtu amwone kiongozi wake mpendwa mara ya mwisho.

Upenzi huo ndio pia ulifanya Mwalimu Julius Nyerere akafunuliwa, Benjamin Mkapa akafunuliwa, John Magufuli akafunuliwa na Edward Sokoine akafunuliwa, wananchi wakaziona sura zao kwa mara ya mwisho kwani kuna umuhimu na uzito wake.

Lakini kutokana na hayo yaliyojiri katika maisha ya Lowassa ambaye hakutaka kujibu kila tuhuma alizosukumiwa, aliona ni bora akaonwa na familia yake na si kila mtu, kwani katika msafara ule wa mamba, kenge walikuwamo wa kutosha. Alale pema peponi Laigwanan Edward Ngoyai Lowassa.

## HABARI PICHANI

# MAZIKO YA WAZIRI MKUU MSTAAFU HAYATI EDWARD NGOYAI LOWASSA KATIKA PICHA



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi wengine katika maziko ya Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa, kijijini Ngarash, wilayani Monduli, mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akimfariji mjane wa Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Mama Regina Lowassa wakati wa maziko. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa akiweka shada la maua kwenye kaburi la Hayati Edward Ngoyai Lowassa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Sehemu ya waombolezaji waliohudhuria maziko hayo. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akiweka udongo kwenye kaburi la Hayati Edward Ngoyai Lowassa. **PICHA: IKULU**

# MAISHA

FEBRUARI 18, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana


Jumapili





# REFUSHA NYWELE KIASILI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | | U | M | E | M | E |
| A | | | | L | | N |
| N | | M | E | E | | D |
| E | P | A | | Z | E | E |
| S | | T | A | A | | S |
| C | | A | | | | H |
| O | N | A | N | A | | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DOM, ILE, BUU, LOA, UKAME, AIMBE, DAIMA, URAIA, MWALIMU, ANGUKIA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI








## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Watoto wawili walikuwa wakigombea mapera, mama mmoja alitokea na kuwaamulia na kuwataka kila mmoja kusema tatizo ambalo limewafanya kugombana.

Juma: John ndiye mgomvi alinipora mapera yangu

John: Hapana yeye ndiye mgomvi alichukua mapera katika mti aliopanda baba

Juma: Ule mti umejiotea pale msituni, huyu ni muongo

Mama: Nyinyi wote nawaona mnadanganya ugomvi haufai kwa sababu huleta chuki

John: Kweli mama hata mwalimu alisema heri nusu shari, kuliko shari kamili

SWALI

Je sukari inayotumika nyumbani inatengenezwa kutokana na zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mke wangu ana roho mbaya sana, nichukue uamuzi gani?

KARIBU msomaji tuendelee na vitimbwi ndani ya ndoa. Hebu tafakari ujumbe huu, na maoni pia ushauri wa wadau kuhusu jambo hilo. Msomaji wetu mzuri ana kilio kifuatacho;-

"Naishi na mke wangu miaka 10, mke huyu ana roho mbaya sana, chake ni chache, changu ni chake, hapendi watoto wangu, tunapoishi hafiki mtu yoyote wa upande wangu awe rafiki au ndugu nimefanya anavyotaka, nilikuwa dini nyingine kwa sasa ni Mkristo lakini haridhiki.

Nataka nimfanyie ubaya apoteze maisha lakini roho inakataa, nyumba tumejenga wote lakini anajifanya ni ya kwake, nifanyeje nyumbani amejaza ndugu zake. Je, dada Flora hata unyumba ni shida yuko busy na ndugu zake. Pia jua kuwa hatuna mtoto na huyu mama naomba ushauri wako kabla sijaua nikafungwa".

Mpenzi msomaji, huo ndio ujumbe wenyewe. Naam. Ukimuona mtu mzima anatoa machozi, ujue yamemfika makubwa. Ujumbe huo niliuweka kwenye WhatsAPP yangu na yafuatayo ni baadhi ya maoni ya wadau.

Mmoja akasema; "Jamaa mwenye mke mwenye roho mbaya achukue uamuzi wa busara na mgumu amwache huyu mke na achukue watoto wake amwachie nyumba na kila kitu ndani achukue nguo zake na wanae akaanze maisha upya kwa maslahi ya watoto wake.

"Akimfanyizia atakamatwa na hata kufungwa, wanawe watahangaika zaidi. Akumbuke yeye na mkewe siyo ndugu, lakini yeye na wanae ni damu moja. Kama akianza maisha mapya asiishi na mwanamke ambaye ana uhusiano naye kimapenzi mpaka wanae wawe na umri wa kujitegemea labda mama mzazi wa wanawe.

"Au ajifunze kuishi naye na hayo manyanyaso kwani ndoa za siku hizi ili zidumu lazima upande mmoja ukubali kunyanyasika." Hivi ndivyo anavyomaliza ujumbe msomaji huyu.

Mwingine akasema; "Dah! Hali inatisha dada Flora ila namshauri asifanye uamuzi wa hivyo isije ikawa ndio mwisho wa maisha yake. 'Ni hivi kama wamefunga ndoa, ajaribu kutafuta wazee wa pande zote wajadiliane kuhusu matatizo yao kupata ufumbuzi wa kudumu. Najua haliwezi kushindikana. "Nasema tena asiamue kuua, amuombe Mungu tu maisha yatajakuwa mazuri". Steven Nestory Mugalula, Morogoro.

Ujumbe mwingine unasema, "ushauri wangu kwa jamaa ni kwamba asichukue sheria mkononi bali apeleke malalamiko kwenye vyombo vya sheria". John Augustine, Mwanza

Msomaji mwingine ujumbe wake unasomeka, " ndugu yangu hawa wanawake watatuua, usihofu kabisa wewe mlete mama yako au baba yako ukae naye hapo atakapoanza kuonyesha ubabe wake ndipo patamu pa kufika kwa mchungaji na kuvunja ndoa, mama huyo ni muuaji. Usihofu kupoteza nyumba maana najua mtagawana ila poa tu ili mradi umeachana na mtu kama huyo. Alfonce Colman, Mbagala, Dar.

Mpenzi msomaji, hizo ni baadhi ya ujumbe uliowasilishwa kwenye dawati la safu hii kuhusiana na kilio cha msomaji wetu mzuri wa gazeti la Nipashe Jumapili.

Binafsi, naungana na wale wanaokubali kuwa hilo ni tatizo lakini linahitaji kutatuliwa kwa busara bila hasira ili kuepusha madhara kama vile kuua na kadhalia. Ni kweli kama walivyosema baadhi ya wasomaji kwenye maoni na ushauri wao kwamba badala ya kuchukua sheria mkononi ni vema ufumbuzi ukapatikana kwa njia ya mazungumzo.

Mazungumzo hayo yahusishe wazee wa pande zote mbili pamoja na washenga ili kusikiliza chanzo cha tatizo na kufikia maamuzi ya busara pasipo kuonea upande wowote. Zipo sheria zinazoweza kutoa suluhisho kama vile sheria ya ndoa ya mwaka 1971 na pia Sheria ya Mirathi.

Kwa kuwa ameishi na mke huyu muda mrefu, basi ajiandae kugawana walizochuma pamoja, kisheria, la asamehe amwachie akaanze maisha ya amani kwingine.

Na kama zipo mali alizochuma kabla ya kuoa, ana hiari ya kugawana na mama huyu au ana hiari ya kutomgawia. Kadhalika mama huyu kama mali anazo kabla ya kuolewa, hizo ni zake na halazimiki kugawana na mumewe. Ndivyo sheria ya ndoa inavyotuambia.

Msomaji wangu, bila shaka umewasikia wenzetu hao kupitia ujumbe mfupi wa simu. Kama nawe una maoni kuhusu suala hilo usikawie kunijulisha kupitia simu ya safu hii.

**Je, una maoni, Kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Chokochoko zako kwa mabinti, umewashtua wajengee chini

UKIZOEA vya kunyonga, vya kuchinja huviwezi. Aisee! Acha tu nikwambie ukweli, wivu sina ila roho inauma.

Bi mkubwa eeh! Ukizoea kuishi maisha yasiyo yako ni ngumu sana kuwa na stara. Unajishusha hadhi na unakosa ule uhalali wa kuonekana mtu aliyestaarabika na mwenye ukomavu wa akili.

Sawa! Wewe ni mama mwenye nyumba lakini hivi unawataka nini wasichana au mabinti waliopanga nyumbani kwako? Maana kila iitwapo kesho, visa, chuki na ugomvi haviishi.

Una nini lakini? Mara sitaki mpangaji mwenye watoto zaidi ya wawili, mgeni akikutembelea mwisho siku tatu nataka aondoke. Mara wanpangaji mnanijazia choo changu. Woii, mara sihitaji wapangaji waliooa.

Hivi unajua kwamba wengi wetu tunaishi na wewe hapa kwa akili tu na huko mtaani tunajengea nyumba chini. Kwa ufupi ni kwamba tunao uwezo wa kujenga na kumiliki mijengo na vyumba vya kupanga kama wewe. Upo hapo!

Una matatizo mengi sana wewe mama mwenye nyumba. Yaani umeamua kupandisha kodi ya pango ili kunikomoa nihame kisa una wasiwasi na mumeo.

Halima, huo si ustaarabu hata kidogo. Usinyanyase wapangaji, wote tungekuwa na nyumba nani angepanga?

Halafu kitu kingine, usianzishe vita kabla ya kupima gharama, kwa vile hata wanasaikolojia wengi duniani, wanaamini kwamba kufuata njia ya amani kuna faida zote.

Kufarakana huvuruga aina zote za mafanikio, maendeleo na kufunga milango yote ya baraka zako.

Kama ni hofu ya tunda la mumeo kuchukuliwa, jitenge na vita ya wapangaji wa kike. Omba busara ikutangulie maana wapangaji hao hao watamiliki nyumba na kubiringita magari ya pesa nyingi ukiwa hapo hapo.

Furaha haitibu majeraha lakini angalau inawanyima maadui zako mahali pa kuanzia, wakati upitapo kwenye majaribu. Si ndiyo eeh!

Mara Harrier imepaki mlangoni, mara kanunua viwanja karibu na makazi yako. Jamani jamani, usiombe Mungu akageuza kibao, mbona utajuta.

Mtu wa aina hii hafai kwenye manowari ya kivita kwa sababu amekaa kimaslahi zaidi. Huyu mama mwenye nyumba kama kusema au kufanya lolote kutampa fursa, basi atatenda.

Suala lingine ni kuhusu mikataba kati ya mpangaji na mwenye nyumba. Wenye nyumba hujiamulia kukatisha mkataba wakati wowote bila kujali mpangaji anaathirika kiasi gani wala kujali makubaliano ya mkataba huo.

Kisheria, mwenye nyumba anapokatisha mkataba anatakiwa amlipe fidia mpangaji.

Kodi ya pango ni mdudu ambaye hunyanyasa wengi hasa wa kipato ha chini. Kila anayemiliki nyumba katika maeneo ya mijini hasa hasa katika majiji,manispaa na miji hakika anaitwa Halima mbarikiwa.

Anaitwa Halima mbarikiwa kwa sababu nyingi. Kwanza, ardhi ni kitu cha thamani, pili, ujenzi ni gharama na anayefanikiwa, hakika huyo amejikwamua kiuchumi na kijamii.

Wamiliki wengi wa nyumba wako katika makundi kadhaa, kuna wanaoishi katika nyumba zao bila kupangisha na wengine wanaozikodisha na kujipatia fedha.

> **Kama ni hofu ya tunda la mumeo kuchukuliwa, jitenge na vita ya wapangaji wa kike. Omba busara ikutangulie maana wapangaji hao hao watamiliki nyumba na kubiringita magari ya pesa nyingi ukiwa hapo hapo.**

Wenye nyumba wengi wamekuwa kama miungu watu. Baadhi yao wamejivika kilemba cha utukufu na kutumia rasilimali zao kwa unyanyasaji wa hali ya juu. Halima wewe una nini lakini?

Best, unajua kwamba sheria zipo, bali hazina meno! na kama zina meno basi meno hayo si makali.

Kwa mfano, mwaka 1999 Bunge lilipitisha sheria mpya kabisa ya ardhi. Ya kwanza ni ile Namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999. Kabla ya sheria hii ilikuwapo sheria ya udhibiti wa pango ya mwaka 1984 ambayo ilihusika na nyumba za kupanga.

Vilevile, ilijumuisha nyumba za biashara, kubwa na ndogo, binafsi pamoja na nyumba za umma.


Baadaye, mwaka 1992, sheria hiyo ikigawanywa na mashiriki ya umma na taasisi yakaondolewa kuwa chini ya sheria hii.

Chini ya sheria hii kuna baraza la utatuzi wa migogoro ya wapangaji na wenye nyumba.

- **Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI







**ILIKUWA siku ya furaha kwa Dk. Mauma Joseph na mkewe Sophia Ndosy baada ya kufunga ndoa katika Kanisa la Waadventista Wasabato Nyegezi jijini Mwanza, ndoa hiyo ilifungwa Desemba 10, mwaka jana.**



# MITINDO







## SWETA LA KUFUMA

SWETA la kufuma kwa mikono licha ya kuwa na mwonekano wa kisanaa zaidi, lakini moja ya mitindo ya mavazi inayopendekeza kutazama.

Kumekuwa na mageuzi mapya katika ubunifu wa kuyaunda masweta ya aina hii na kufanya kila mtu kutamani kuwa nayo.

**UTATOKAJE?**

Nguo hizi ambazo zinavaliwa sana nyakati za baridi, hata hivyo utaonekana mjanja ukipigilia kwa mchanganyiko wa mavazi mengine kama suruali na buti zenye visigino virefu.

Hata hivyo, unapovaa sweta za kufuma zinakupa machaguo mengi ikiwamo suruali ya jeans nyembamba.

Upande wa wasichana wanaotaka kutoka tofauti, mchanganyiko wa sweta na sketi fupi itasaidia kurekebisha mwonekano wao na kuwa wa kisasa zaidi.

Vazi hilo linapendeza zaidi kama utavaa viatu vyenye visigino virefu au raba zenye muundo wa kisasa.

URMEBO

Na Mary Geofrey



# REFUSHA NYWELE KIASILI

NYWELE ni moja ya sehemu ya kiungo muhimu katika kuongeza urembo kwa wanawake na kumuweka utanashati kwa wanaume.

Kila mtu ana utashi wa kuona anazo nywele nzuri, ndefu na zenye afya.

Hata hivyo, kuna baadhi ya watu wana tatizo la nywele kutorefuka yaani kudumaa na kusababisha kupoteza sifa ya kuwa na mwonekano mzuri.

Leo unaweza kujifunza namna ya kutumia matunda na asali kurefusha nywele zako

**Namna ya kutengeneza**

Chukua parachichi kubwa moja, asali vijiko vitatu na kiini cha yai.

Osha nywele zako kwa shampoo na kisha uzikaushe.

Ponda ponda parachichi mpaka lilainike kabisa. Chukua vijiko vitatu vya asali na kiini cha yai kisha changanya yote kwa pamoja.

Paka mchanganyiko huo kaa nao kwa muda wa dakika 15 kisha osha.

Fanya hivyo kwa muda wa wiki moja hadi mbili na utaweza kuona matokeo mazuri katika nywele yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Umeshakula mkate wa mayai?

MKATE wa mayai unaweza kuupika nyumbani na kufurahia mlo na familia yako.

**Mahitaji**

Mayai manne, sukari vijiko viwili na nusu, unga wa ngano vijiko sita vya chakula, hiliki iliyosagwa nusu kijiko cha chai na backing powder nusu kijiko cha chai.

**Jinsi ya kupika**

Chukua bakuli safi, weka ndani yake sukari na hiliki, kisha vunja mayai yote juu yake.

Changanya mayai, hiliki na sukari, kwa kutumia mashine (cake mixer), mpaka sukari ivurugike na mayai yapande juu kama povu.

Paka mafuta chombo chako cha kuokea mkate na washa jiko lianze kupata moto.

Tia baking powder katika unga wako, kisha chukua mwiko na uanze kutia unga kidogo kidogo katika mchanganyiko wako wa mayai na sukari umekamilika. Hakikisha unaukoroga vizuri kila utiapo unga ili kuepusha kuwa na madonge.

Mimina mchanganyiko wako katika chombo cha kuchomea mkate.

Oka mkate wako ndani ya jiko au oveni kwa muda wa kama dakika 20 kisha utoe na ukipoa utakuwa tayari kwa kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Mambo muhimu ujenzi wa nyumba imara

UIMARA wa nyumba ni kuhimili mambo mengi ikiwamo changamoto zinazojitokeza katika nyakati za mvua, upepo mkali pamoja na uzito wowote unaoipiga.

Alfred Marko, anajishughulisha na masuala ya ujenzi wa nyumba na anasema uimara na uzuri wa nyumba unategemea vitu vingi.

Kwamba, kwa nyumba za kawaida, uimara wake huanzia kwenye ujenzi wa msingi, kuta, paa, nguzo, mihilimi, milango, madirisha na dari. Yote haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa ujenzi wake.

"Nyumba imara na mwonekano mzuri ni alama kwa eneo husika, huongeza thamani ya jengo, madhari ya jengo iliyowekwa katika uzuri, pia huleta hisia na utulivu, furaha na uchangamfu kwenye familia na mtaa,"anasema Marko.

"Ni muhimu jengo liwe imara na uzuri unaoendana na matumizi yake, kama ni kwa ajili ya biashara, basi liwe lenye mvuto unaovutia hata wateja, kama ni kwa ajili ya kuishi familia, basi ichangie kuleta amani na furaha nyumbani," anaongeza.



Anashauri kwamba ni vema nyumba ikafanyiwa usanifu mzuri na bora kuanzia jengo lenywe, mazingira ya ndani, madhari ya nje ili yabebe maana fulani na kwamba ni muhimu kuwa makini na maana hiyo unayomwambia mtu kupitia nyumba yako.

"Rangi, mpangilio, mpishano, kimo, ukubwa, umbile la nyumba yako huathiri hisia za mtumiaji. Pia niwakumbushe kwamba rangi nyeupe kwenye nyumba huleta hisia za usafi, utaratibu na amani.

"Kijani huleta hisia za utulivu, uasili. Nyekundu huleta hisia za kusisimua, shauku, changamfu. Rangi ya waridi huleta hisia ya furaha na ya bluu huleta hisia za uasilia na utulivu pia, kwa hiyo ni muhimu kufanya chaguo sahihi unapopanga au unapokamilisha ujenzi wa nyumba ya ndoyo yako," anasema.

Anashauri kwamba jambo la msingi ni kujenga nyumba unayohitaji, itakayokidhi mahitaji ya sasa na baadaYe, yenye usalama na uimara, iliyo katika uzuri wake na kuepuka kujenga usiyoihitaji.

Kufahamu aina ya nyumba inayokufaa kujenga ni miongoni mwa jambo linalosisitizwa na mtaalam huyu kwa kuwa ndiye mahali muhimu ambapo kila mtu anapatia faraja na kupata muda wa kupumzika baada ya shughuli nyingi za kujitafutia kipato.

DONDOO

## Tengeneza eneo la 'kibenchi' nyumbani

**Na Restuta James**

WATAALAMU wa mapambo wanaeleza kuwa haijalishi eneo lako la nyumbani ni kubwa au dogo kiasi gani, lakini ukiamua unaweza kujitengenezea sehemu ya kupumzika.

Wanaeleza mbinu rahisi na nafuu za kuongeza utulivu uwapo nyumbani kwako hasa kwa wenye eneo dogo la bustani.

Mtaalamu wa mapambo, Gaudensia Massawe, anasema mtu mwenye eneo dogo anaweza kutumia sehemu ya ukuta wa nyumba au fensi kutengeneza bustani au mimea dawa/viungo.

Anasema anaweza kutumia maturubai maalumu kama yanayotumika kwenye eneo la maegesho ya magari nyumbani, kuandaa mazingira ya kivuli na kutengeneza kibenchi cha mbao tupu au mbao na chuma au chuma tupu na kukiweka eneo hilo.

"Hapo unaweza kuweka maua ya kuning'inia au mimea mahsusi kama rosemary na coriander pamoja na maua machache ya kupandwa chini," anaeleza Gaudensia.

Anashauri kutengeneza sehemu ya kuning'iniza maua yako iwe katika mwonekano wa kisasa kwa kuweka fimbo za chuma ambazo unaweza kupaka rangi uipendayo huku akipendekeza nyeupe.


"Unaweza pia kutengeneza shelve kimtindo kwa kuweka uwezekano wa kuweka makopo mawili yasiyo ning'inia na mengine yakaning'inia ili kuongeza nakshi," anasema.

Anasema ili kuweka ukisasa na uzamani, katika eneo hili, mwenye nyumba anaweza kuweka vyungu vya kufinyangwa kuliko kuweka makopo ya kisasa ya plastiki

Anasema eneo hili unaweza kupanda nyasi, kuweka changarawe au kokoto kulingana na kile unapenda.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
PEPO LA NGONO TOKAAA AMKUMBUKE MKE NA WANAWE AKIPATA MSHAHARA AUSALIMISHE AENDE NAO KWAKE
SIJUI NITAPITA NAO NJIA GANI HADI UFIKE SALAMA!
MBONA HUSEMI UNAHAMIA WAPI ZAIDI YA SIMU ZAKO KUWAHAKIKISHIA WENYEJI WAKO WATAFURAHI?
NAHAMIA N'TWARA
HUYU SI NTU!
NIME'NSIKIA!
ASEE ALIYEPIGWA KIBAO AKAZIMIA KAAMKA NA YUPO ANADUNDA KAMA HAKIJATOKEA KITU!
LILE NI SOMO TUPUNGUZE SHOBO KWENYE MISAFARA
MIMI NILIKUWEPO PALEPALE ILE INGEKUWA NGUMI NDUGU WANGEFUFUNGA TURUBAI MANAKE UPEPO TU, MIE CHALI'
ULIKUWEPO WAPI ACHA MAUJIKO YASIYO NA MAANA EMBU KAA KIMYA!
KILE SIO KIBAO ILE NI NGUMI AINA YA 'SHINGHA' WANAITUMIAGA SANA WACHINA
MSIKUZE MAMBO MIMI NIMEMUHOJI YUPO 'MWAISELA' KAENDA KUMUONA MGONJWA WAKE AMELAZWA!
WEWE UNAYEMNYAMA-ZISHA MWENZAKO USIJE UKASEMA WEWE NDIO "MKONO WA CHUMA" SISI TUMEMKARIRI UFANANI NAE HASILANI!
BORA UMEMKATA UMEME
MBAGALA
WEWE KULA UENDE MIMI MKE WA MTU NIMEOLEWA KWA NDOA
USIMALIZE MANENO NILIKUWA NAKUTESTI TU NIONE KAMA BADO NAJUA KUTONGOZA
UMEALIKWA?
AMMA!!! MWALIKO WA MSELA UKAUZU WAKE'
NASKIA ULIKUWA UNATAKA KUJIUA ULIPOSIKIA NIMEPEWA LIFTI NA MTALAKA WANGU!
HUYO ALOKWAMBIA KAMA NI MWANA'NKE ANANTAKA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KATAFUTE SIFA UKWENI MAKOSA YAKO APEWE MKEO...

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Sall akubali kuitisha uchaguzi mkuu Senegal

**DAKAR,** SENEGAL

SIKU mbili baada ya Mahakama ya Katiba kutengua agizo la kuahirishwa kwa uchaguzi nchini Senegal, Rais Macky Sall ametangaza kutekeleza hukumu hiyo haraka.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari ilisema kiongozi huyo amejitolea kutekeleza bila kuchelewesha mashauriano ya kuandaa uchaguzi mkuu katika muda muafaka.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo raia wa taifa hilo walisubiri kujua lini na jinsi gani zoezi la upigaji kura utafanyika.

Hata hivyo, kauli ya kiongozi huyo imetoa matumaini kwa kufanyika uchaguzi huo katika muda unaokubalika.

Taarifa hiyo ilisema kwamba Rais Sall ananuia kutekeleza kikamilifu uamuzi wa Baraza la Katiba na bila kuchelewa atafanya mazungumzo kwa ajili ya kuandaa uchaguzi wa haraka iwezekanavyo.

Aidha, taarifa hiyo iliongeza kwamba Rais Sall amechukua maelezo ya uamuzi huo wa Baraza la Katiba ambao uko ndani ya mfumo wa taratibu za kawaida za mamlaka.



Waandamanaji wakiweka maua na mishumaa nje ya ubalozi wa Russia jijini Zurich nchini Uswiz kuomboleza kifo cha Navalyn jana. **PICHA: REUTERS**

# Viongozi Afrika waanza mkutano Ethiopia

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

VIONGOZI wa nchi mbalimbali barani Afrika, wanashiriki katika mkusanyiko wa mkutano wa Umoja wa Afrika (AU) ilioanza jana.

Mkutano huo unafanyika katika mji mkuu wa Ethiopia wa Addis Ababa, unatarajia kujikita matatizo yanayolikumba bara hilo ikiwamo vita, ukosefu wa usalama na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Aidha, katika mkutano huo viongozi hao watajadili suala la Elimu masuala mengine ikiwemo mgogoro wa Ukanda Gaza.

Bara la Afrika linakabiliwa na mizozo ya kisiasa kuanzia Sudan, Senegal hadi eneo la Sahel, hakuna utulivu, huku mivutano ya kisiasa imezidi kuathiri raia.

Mkutano huo ambao huanza na shamra shamra ambazo huambatana na vikao vya viongozi wa bara hilo, changamoto kubwa ni umaskini miongoni mwa raia pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Umoja huo unalalamikiwa kutokuwa na meno katika kushughulikia matatizo ya Afrika.

Karibu miezi miwili baada ya mkutano wa mwaka jana, Sudan ilitumbukia katika mgogoro wa mapigano na inasubiriwa kuangalia iwapo mkutano wa mwaka huu utatoa suluhisho.

**DW**

# Viongozi wa ujasusi DRC wakamatwa kusaidia M23

**GOMA,** DRC

MKURUGENZI wa ujasusi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (ANR) katika mkoa wa Kivu Kaskazini, manaibu wake wawili na msemaji wa gavana wa mkoa huo wamekamatwa kwa tuhuma ya kuwasaidia waasi wa M23

Watu hao wamekamatwa Februari 13 na kupelekwa mji mkuu wa Kinshasa, ambako wanazuiliwa wakiendelea kuchunguzwa. Kurugenzi Kuu ya Ujasusi wa Kijeshi inawashutumu viongozi hao kwa kuhusika na kusaidia waasi wa M23, unaoungwa mkono na Rwanda.

Kulingana na kituo cha Radio cha OKAP cha nchini DRC, kitengo hicho cha jeshi la taifa kilichukua hatua hiyo baada ya kunasa mawasiliano kati ya watuhumiwa na waasi wa M23.

Msemaji mpya wa gavana wa kijeshi wa mkoa wa Kivu Kaskazini, ambaye aliteuliwa wiki chache zilizopita, alikuwa kada wa chama cha kisiasa cha Corneille Nangaa, na alijiondoa katika chama hicho muda mfupi kabla ya uchaguzi.

Alipohojiwa kuhusu suala hilo, msemaji wa kijeshi wa Gavana wa Kivu Kaskazini, Luteni Kanali Njike Kaiko alisema bila kutoa maelezo zaidi kuwa faili hili limefikishwa mahakamani.

Kukamatwa kwa viongozi hao kulifanyika wakati mapigano makali yakiendelea kati ya jeshi la serikali na waasi wa M23, katika maeneo ya Sake na Masisi.

**RFI**

# Viongozi duniani wamlilia Navalny

**WASHINGTON,** MAREKANI

KUFUATIA kifo cha kiongozi wa upinzani nchini Russia, Alexei Navalny, kilichotokea gerezani kimesababisha mamia ya watu katika majiji duniani kuingia barabarani kuandamana.

Wafuasi wa mwanaharakati huyo wa kisiasa mwenye umri wa miaka 47, walikusanyika nje ya balozi za Russia katika majiji makubwa ya nchi za Ulaya ikiwamo London, Paris, Geneva na New York.

Mjini Berlin, umati mkubwa wa watu ulipiga kelele kumlaani Rais Vladmiry Putin wakiomba apelekwa mahakama ya kimataifa ya jinai ya Thei Hague kama mtu aliyesababisha kifo hicho.

Zaidi ya watu 100 walisimama mbele ya jengo la makao makuu ya Umoja wa Mataifa, mjini Geneva na kushikilia picha za Navalny na kuweka maua.

Pia kulikuwa na maandamano nchini Russia na picha zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zilizoonyesha vikundi vya watu wakiweka maua kwenye makaburi ya muda huko Moscow na Saint Petersburg.

Taarifa zilieleza kwamba zaidi ya watu 100 wanaripotiwa kuzuiliwa katika miji mbali nchini humo.

Alexei Navalny ni mmoja wa wanasiasa mashuhuri wa upinzani nchini Russia na alifungwa jela kutokana na makosa ya kisiasa.

Wakati huohuo, Rais wa Marekani Joe Biden, amemtuhumu Putin kwamba ndiye anahusika kwa kumuua mwanasiasa mpinzani.

Juzi Jeshi la magereza katika eneo ambalo Alexei Navalny alikuwa akitumikia kifungo chake lilitangaza kifo chake bila kutaja chanzo.

“Kilichotokea ni ushahidi mwingine wa ukatili wa Putin,” alisema Biden.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, David Cameron alisema kuwa hakuna mtu anayepaswa kuwa na shaka yoyote kwamba utawala wa Putin ni mbaya kwa kile kilichotokea.

Nchi ya Ufaransa ilisema Navalny alijitolea maisha yake kwa kusimama dhidi ya ukandamizaji, na Waziri wa Mambo ya Nje wa Norway alisema mamlaka ya Russia ilihusika katika kifo chake.

Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama, amemtaja Navalny kuwa mtetezi asiye na woga wa imani yake ambaye alikufa bila kuvunjwa moyo na ukatili aliopinga.

Obama alisema alipambana na ufisadi, alihamasisha mamilioni ya watu na kamwe hakutetereka katika msisitizo wake wa uhuru wa kujieleza, utawala wa sheria, na Russia inayowajibika kwa watu na sio dikteta.

**BBC**

## MAKALA

# MAISHA, KIFO CHA EDWARD LOWASSA NI FUNZO KWETU



Na Magabilo Masambu

**Baada ya kukatwa, hakukata tamaa alihamia katika siasa za upinzani, mara hii alitimkia CHADEMA, chama ambacho kilikuwa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), umoja usiyokuwa rasmi wa baadhi ya vyama vya siasa vilivyoamua kujiunga ambavyo mbali na CHADEMA ni Chama Cha Wananchi (CUF), NCCR- Mageuzi na National League for Democracy (NLD).**

KUNA mambo katika maisha hutokea si kwa bahati mbaya bali huwa yanakusudiwa kutoa somo. Vilevile kuyasema mambo hayo si kukusudia kufukua makaburi bali kwa ujumla wetu, tupate muda wa kutafakari mienendo yetu kwa kuzingatia utamaduni wa Kiafrika hasa wa Kitanzania.

Edward Lowassa alikuwa kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa muda mrefu, mbunge wa Monduli takriban vipindi vinne na amekuwa waziri katika baadhi ya wizara na Waziri Mkuu wa tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya mwaka 2006 na 2008 alipojiuzulu wadhifa huo.

Mwaka 1995 alikuwa miongoni mwa wanachama wachache wa CCM waliochukua fomu ya kuwania urais wa Tanzania lakini kwa bahati mbaya hakupata nafasi hiyo. Benjamin Mkapa, ambaye kwa sasa ni marehemu, ndiye aliyepitishwa na chama na hatimaye kuwa Rais wa Awamu ya Tatu, akitanguliwa na Mwalimu Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi.

Miaka 20 baadaye, Lowassa akajitokeza tena kutangaza nia kupitia chama chake lakini kama wasemavyo Waswahili, ng'ombe wa masikini hazai na akizaa huzaa dume, Lowassa hakufanikiwa kuruka viunzi ndani ya chama chake kama ilivyotokea mwaka 1995.

Baada ya kukatwa, hakukata tamaa alihamia katika siasa za upinzani, mara hii alitimkia CHADEMA, chama ambacho kilikuwa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), umoja usiyokuwa rasmi wa baadhi ya vyama vya siasa vilivyoamua kujiunga ambavyo mbali na CHADEMA ni Chama Cha Wananchi (CUF), NCCR- Mageuzi na National League for Democracy (NLD).

Kitendo cha Lowassa kuhamia upinzani hakikuwapendeza wengi ndani ya chama chake, lakini vilevile baadhi ya watu ndani ya UKAWA. Ndani ya UKAWA wako walioamini kwamba anakuja tu kama mwanachama ili kuongeza nguvu lakini baadaye mambo yakabadilika akapewa nafasi ya kupeperusha bendera ya ukawa kupitia CHADEMA.

Kwanza, kwa mujibu wa sheria, Lowassa hakuwa amevunja sheria yoyote ya nchi, hivyo aliamua kutumia uhuru wake wa kikatiba kufanya alichoona ni chema na ni uamuzi mzuri kwake. Kampeni kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2015 zikaanza, kila mtu anaweza kuwa shuhuda umati aliokuwa nao Lowassa katika mikutano yake, upande wa pili Dk. John Mgufuli naye akatisha kweli kweli. Kwa hiyo kukatokea mchuano mkubwa kati ya wagombea hao wawili.

Jambo la hovyo likaanza kujitokeza katikati ya kampeni. Baadhi ya watu wakaanza kumshambulia Lowassa kwa maneno yanayomhusu yeye binafsi na hasa la afya yake. Wako waliosema sana, wapo waliomtukana na wako walioandika. Pamoja na maneno yote hayo, Lowassa hakuwahi kunukuliwa ama kusikika mahala popote akijibu mashambulizi hayo.

Wakati fulani akiwa na waandishi wa habari, akaulizwa kuhusu kusemwa sana na hasa kuhusu afya yake, alijibu maneno machache sana kwamba: "Aliyewapa afya wao, ndiye aliyenipa ugonjwa." Baada ya hapo akaendelea na kampeni.

Tofauti na baadhi ya wanasiasa wengi, Lowassa akiwa CHADEMA, hakuwahi kusikika akikisema vibaya chama chake cha zamani (CCM) na hata aliporejea CCM hakuisema vibaya CHADEMA. Aliwashukuru viongozi wake na wanachama kwa ujumla na mpaka Rais Magufuli alikiri kwamba Lowassa ni mtu wa aina yake.

Kifo chake kimekuwa funzo kwetu kwa sababu baadhi ya wale walioonekana kumsema kwamba walikuwa na afya njema, walishatangulia mbele ya haki, mmoja baada ya kuandika gazetini nilimpigia simu kumuuliza kulikoni? Na sasa Lowassa amekuwa kama mtu wa mwisho kwao. Hapa tuna jambo la kujifunza kwamba, afya ya mtu ni Mwenyezi Mungu ndiye anayeweza kuamua nani aanze na nani abaki.

Haya lazima tuyaseme hata kama ni magumu ili yatusaidie huko mbele tukizingatia kwamba mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mitaa na mwaka kesho tuna uchaguzi mkuu. Hatutarajii kusikia kuzungumza watu badala ya hoja. Tunataka kusikia ukiwa kiongozi utashirikianaje na wananchi katika kutatua changamoto za maendeleo.

Najua sasa hivi kuna watu wanajipanga kuchafua wengine kwenye majukwaa lakini sidhani kama ni aina ya siasa ambazo Watanzania wanazihitaji. Wako watakaotumia jinsia na mengine lakini ndugu zangu tujifunze kilichotokea mwaka 2015. Vilevile ni muhimu kuwa na akiba ya maneno hasa wanasiasa vijana. Tusirithi maadui wa watu wengine tukacheza ngoma tusiyoijua.

Nayasema haya kwa nia njema kabisa, maana nimesikia kila mtu akimwongelea vizuri Lowassa, safi lakini uzuri wa mtu usiwe tu anapofariki dunia. Kama ni kweli tunamaanisha, tusingelisikia yote yale tuliyoyasikia majukwaani, vinginevyo tuamini kwamba mengi yalikuwa ya kutunga, jambo ambalo pia si jema. Tuwe na siasa halisi na Mwenyezi Mungu atatutasidia kuijenga nchi yetu kwa pamoja.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mpenzi wake ana sura mbaya, kweli lakini yanakuhusu nini?*



Na Adam Fungamwango

**Lakini ukiona msukosuko, mara mpenzi wako kapelekewa maneno kuwa, 'mwanaume gani yule hana pesa, ana wanawake kibao hapa mtaani, ulipendea nini yule?' Ujue lishikilie sana hilo penzi, kuna watu linawakera, linauma.**

MUME wake mfupi. Ni kweli lakini yanakuhusu nini? "Ana makengeza." Ndiyo lakini mwenyewe amempenda hivyo hivyo. "Mbona Rehema kaenda kuchukua mwanamume mweusi vile?" Ndiye huyo aliyemchagua.

Ndani ya jamii kuna baadhi ya watu ambao kazi yao ni kujadili maisha ya watu. Kuna waliojipambanua, wao wanadili na mambo ya mapenzi ya watu tu.

Achana na wale ambao wanajadili maisha ya kila siku, ameamkaje, amekulaje, ana pesa, hana, amemkopa nani na vitu vingine vinavyofanana na hivyo. Sasa hao ninaosema mimi leo ni waliojikita kwenye umbea, upande wa mapenzi. Wanataka kujua fulani mpenzi wake nani.

Wakishajua wanafuatilia kuona likoje, na wakishaona halina mvuto lipo lipo tu, basi wenyewe watafurahi, watacheza na wapenzi hao watabaki kuwa simulizi tu mitaani.

Tatizo linakuja pale ambapo penzi litaota maua na kuchanua, yakanukia, penzi likawa na mvuto kama maua yaliyotiwa mbolea, lenye mvuto, litaanza kuwauma mioyoni.

Ndani ya jamii ukiona penzi lako halizungumzwi, haliwekewi zengwe, halina misukosuko, badala yake watu wanachekelea tu, ujue kuna sehemu mnakosea. Wanaliona la kawaida tu, halina mvuto.

Lakini ukiona msukosuko, mara mpenzi wako kapelekewa maneno kuwa, 'mwanaume gani yule hana pesa, ana wanawake kibao hapa mtaani, ulipendea nini yule?' Ujue lishikilie sana hilo penzi, kuna watu linawakera, linauma.

Mara nyingi akinadada huwa na hasira za haraka, wao wakiambiwa maneno huwa ni rahisi sana kuamini bila kujua kuwa wanataka kupeperushiwa ndege wao.

Mwanaume naye anaweza kupelekewa zengwe kuwa mpenzi wake ameshatembea na wanaume wengi pale mtaani.

*"Achana naye, kuna wanawake wengi sana tena wastaarabu lakini siyo yule, unamjua vizuri yule ana matatizo sana."*

Mambo kama hayo mara nyingi huwachanganya sana wapenzi ambao hawana msimamo. Wao wanasikiliza zaidi yanayosemwa na watu kuliko wanayosemezana wapenzi wenyewe kwa wenyewe.

Mara nyingi wapenzi huanza kutamkiana kupendana wakiwa wawili tu. Na kama wakitaka mapenzi yao yadumu wasikilizane wao wenyewe tu. Wakati wanapendana hao watu hawakuwepo, kwa nini sasa wawe walimu wa mapenzi ya watu?

Inakuwaje hujui historia ya mpenzi wako na wala hakuna mtu anayekuletea, lakini ikishaonekana mmeingia kwenye mahusiano watu ndiyo wanaanza kuleta mafaili? Tena yake mabaya. Afadhali wangekuwa wanaleta ya aina zote mbili, uzuri wa mtu huyo na ubaya wake. Badala yake unaletewa mabaya kiasi kwamba kama mmoja atakuwa anaamini atagundua kuwa amejitosa kwenye moto wa jehanam na si kupenda mtu wa maisha yake.

Yametokea mengi sana kama haya kwenye jamii. Watu wamepoteza wapenzi wao. Wamelizwa wakalia hadi machozi yakakauka.

Kibaya zaidi baada ya kuamini, baadaye wakaja kugundua kuwa walidanganywa na si walivyoaminishwa. Kurudi tena haiwezekani kwani wapenzi wao wanakuwa wameshapata wengine. Inabaki kilio na kusaga meno.

Bendi ya Amboni Jazz, mwaka 1974 ilirekodi kibao walichokiita 'Wajifanya Wajua', lakini kikaja kuwa maarufu kwa jina la 'Kidomidomi.'

Maudhui ni kwamba jamaa mmoja ambaye amefanyiwa kitendo hicho, amemfuata laivu dada aliyetekeleza mpango wa kuwaachanisha na mpenzi wake, akampasha ukweli.

*"Wewe wajifanya wajue we dada, unakuwa mwalimu ooo wa wapenzi wa watu, mimi nakukanya, usiwe kidomidomi, utakuja aadhirika ulimwenguni humu.*

*Usipende kashifu watu kwa wapenzi wao, utakuja adhirika dada ooo mitaani ooo, huko siko kujenga dada, ni kubomoa. Mimi sikushauri kitu we mama endelea."*

Jamaa mwingine naye akapigwa zengwe mpaka mpenzi wake akawa haeleweki. Sasa kazi imempata ya kumbembeleza na kumwambia aachane na watu fitina watakuja kuharibu mapenzi yao.

Hii inapatikana kwenye kibao kiitwacho 'Kiwele' cha Tancut Almasi Orchestra, mwanzoni mwa miaka ya 1980.

*"Kiwele mimi ni wako wa maisha mama maneno ya watu yasikusumbue mama. Ukifuata ya watu tutakosana bure, tutaharibu ndoa yetu Kiwele.*

*Kiwele heee Kiwele eee, uwe mwangalifu na wambea, Kiwele heee Kiwele eee, jiepushe na watu fitina.*

*Tumependana wawili mimi we, Mola mwenyewe atutenganishe eee, tuliza moyo moyo Kiwele mama.*

*Wamekueleza, eti sina pesa, wamekueleza, eti sina sura, wamekueleza ooo, mume gani huyo, mapenzi hayajali pesa ooo mama, mapenzi hayajali sura ooo Kiwele, mapenzi hayana macho, Kiwele mama ee."*

*Fitina ni mbaya sana, hasa kufitinisha mapenzi ya watu. Waacheni watu walale. Inawezekana ni kweli mtu ni mfupi, mweusi, ana makengeza, lakini yanakuhusu nini?*

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MLANGO ulifunguliwa kwa nguvu kiasi cha kumtisha mpaka Havijawa mwenyewe.

"Unasemaje wewe!?" Ilikuwa sauti kavu ya Sauda iliyochanganyikana na hasira.

Havijawa alilitambua hilo, akashangaa kuona kama wifi yake leo na yeye ameamka kisharishari.

"Unasemaje hiyo vipi? Unanitisha?"

"Siyo nakutisha, huyo kaka yako hataki mimi nimpikie chai alfajiri. Mimi nilikuwa tayari kufanya hivyo, lakini mwenyewe akaniambia ofisini kwake wanakunywa chai, kwa hiyo hapendi kunisumbua mkewe kuamka asubuhi asubuhi, akakataa hata kumpikia usiku na kumuwekea kwenye chupa ili alfajiri aamke. Kama mimi naongopa njoo umuulize mwenyewe. Sitaki mimi kunisingizia uongo."

"Haya na kuzaa nako, maana mwaka unakatika huu hatuoni hata hamu ya kula embe mbichi!"

Hii ndiyo siku ambayo Sauda alikuwa akiisubiri kwa hamu. Alitaka kuufanyia kazi ushauri wa shoga yake Paulina na shoga ya huyo huyo wifi yake ambaye hakupenda tabia ya rafiki yake kumsumbua, kumsema na kumbugudhi mke wa kaka yake. "Hivi wewe mwanamke, kipi ambacho mimi haswa nimekukosea?"

Uulizaji ule na jinsi alivyokuwa siku hiyo ilionekana kabisa kuna kitu amedhamiria. Hata hivyo kwake haikuwa tatizo. "Ahaa hukijui eeee." Sauda akabaki anamtazama kwa kumkata jicho kali wifi yake. Havijana kama kawaida yake naye ni jeuri, hakujali hilo.

"Umenikosea mimi na kaka yangu." Akaendelea kujibu.

"Hivi uchafu, uvivu, utasa wewe vyote unaona sawa hivyo?"

"Unajua wifi mimi nimechoka, ndoa yangu ilikuwa safi wakati wewe hujaja, lakini ulipogusa tu nyumba hii sina amani na ndoa yangu, kwa nini hivi? Sauda naye akarudisha swali. "Umechoka eee, umenichoka mimi, umemchoka kaka yangu, au umechoka kukaa hapa? "Kama umechoka amua tu."

"Nimekuchoka wewe na visa vyako." "Unasemaje wewe?" Tayari Havijawa alikuwa amefura kwa hasira. Akamsogelea ili kwenda ana kumpga ngumi, kibao, au kumvamia.

Sauda ambaye alikuwa tayari kwa lolote siku hiyo alijua hilo. Alijifanya kama amesimama tu anamsubiri. Alipofika karibu Havijawa alimrukia ili amuangushe chini na kuamza kumfumua. Kwa kasi isiyotegemewa, Sauda alimkwepa. Mzima mzima havijana walikwenda kujibamiza kwenye mlango. Akaanguka chini na kuugulia maumivu makali.




**Wakati huo huo, wasichana wanne majirani ambao walikuwa wanasikia ugomvi huo na walikuwa wanachungulia na kukaa tayari kwa lolote litakalotokea, wakafika ghafla. Ilikuwa kama waliambizana, wawili walimkamata Sauda na wawili walikwenda kumnyanyua na kumkamata Havijawa.**

Wakati huo huo, wasichana wanne majirani ambao walikuwa wanasikia ugomvi huo na walikuwa wanachungulia na kukaa tayari kwa lolote litakalotokea, wakafika ghafla. Ilikuwa kama waliambizana, wawili walimkamata Sauda na wawili walikwenda kumnyanyua na kumkamata Havijawa.

"Mnapigania nini jamani mtu na wifi yake?" Akauliza mmoja ambaye alikuwa amemshika Sauda.

"Sijampiga mimi, kajibamiza mwenyewe kwenye mlango. Yeye ndiye aliyetaka kunipiga." Sauda akajitetea. "Niachieni, niachieni nimuonyeshe huyu mpumbavu mkubwa. Na umeyakanyaga wewe, nisikutana na wewe nje, subuleni au mahali popote, nakufumua halafu ukashtaki polisi." Havijawa alipayuka kwa sauti kubwa akionyesha ameumizwa na tukio hilo ambalo hakutegemea.

"Labda ukashtaki wewe, mimi kukupiga naweza ila sitaki tu. Nakuheshimu kwa pua."

"Ahaa kumbe unajiweza eee, tupigane sasa, waambie wakuachie hao tuwekewe mtu kati." Havijana akazidi kuchachamaa huku akirukaruka, akitaka waliomshika wamuachie ili akapambane na wifi yake.

"Na wewe waaambie wakuachie uone!" Akajibu Sauda kwa kujiamini. "Hivi wewe unajiamini nini?"

"Kwani wewe unachoamini nini ambacho mimi sina?" Sauda akamjibu tena.

Waliowakamata waliwakamata mwili na mikono ili wasisogeleane, lakini hawakuwaziba midomo, hivyo vita ikawa ya mdomo badala ya mwili.

************************************

Alikuwa tayari ameshakusanya nguo zake tayari kwa kuondoka. Mabegi mawili makubwa yalitosha kabisa kukusanya nguo zake zote zilizokuwa ndani.

Akaoga, akavaa nguo za safari. Akachukua na kibegi chake kidogo ambacho akinamama hukining'iniza begani.

Akakaa kwenye kochi kumsubiri mumewe. Alisubiri ili amuge. Aondoke kwao. Amechoshwa na visa vya wifi yake. Siku hiyo mumewe alichelewa. Hakujali. Alikuwa na kazi maalum. Ya kumkomesha wifi yake.

Geti lililogongwa na akatoka mwenyewe kwenda kulifungua. Ni yule yule aliyemsubiri. Mumewe Kassim. Akashtuka kuona jioni ile, saa 12:00 hivi mkewe amevaa nguo za safari. "Anakwenda wapi?" Akajiuliza. Alipomtazama sana usoni hakuona ile nuru yake ya kawaida. Akajua tayari kimenuka. Hakutaka kuuliza chochote pale nje. Akasubiri akiingia ndani. Mabegi mawili makubwa, moja likiwa kitandani na lingine juu ya kapeti yalimtisha. "Vipi mke wangu, mbona hivi?" Akauliza.

"Ndiyo vivyo unavyoona. Naondoka!" "Unaondoka? Kwani kumetokea nini?" "Unasikia mume wangu, bora mimi niondoke kuliko siku ukirudi ukute maiti hapa!"

"Kwani kumetokea nini?"

"Kama si majirani basi leo ungekuta maiti moja, au mbili yangu na dada yako! Au basi kama siyo hivyo, mmoja yupo hospitali, mwingine polisi, au wote wawili hospitali!"

"Mmepigana?"

"Nasema hivi, alitaka kunipiga, nimemkwepa, akajigonga kwenye mlango wetu huu. Ana bahati nilitaka nimmalize hapa hapa dada yako. Haiwezekani anitukane mimi na ukoo wangu, yaani sisi kwetu masikini! Ukweli imeniuma sana na kwa hiyo ninachokwambia, naenda kwa dada yangu, nalala kesho asubuhi kwetu, Kondoa."

"Unaenda Kondoa!?" Kassim akashangaa na kushtuka kwa wakati mmoja. "Sasa kwetu wapi? Ulipokuja kukunja goti na kunioa ni wapi? Akaulizwa na mkewe. Wakati akikuna kichwa nini afanye, sauti ya mkewe ikarindima tena masikioni mwake. "Sasa ndiyo utaamua, nani akae hapa, mimi au dada yako. Nakwenda kwetu, nitarudi pale nitakapohakikisha kuwa dada yako hayupo tena hapa."

Ukweli ni kwamba Sauda hakutaka kuondoka. Ulikuwa ni mpango tu ambao ameutengeneza mwenyewe ili kumpa shinikizo mumewe. Alijua akifanya hivyo mumewe atapagawa na kuchukua hatua. Ni kwa sababu anampenda.

Sauti za shoga yake Paulina na shoga wa wifi yake Fatuma walishamwambia apiganie ndoa yake. Asiikimbie kwa sababu ya wifi yake. Sasa alikuwa ameshapanga plani yake. Alijua sasa mumewe, ama yoyote yule mwenye mapenzi mema na yeye anaweza akaamua hili vizuri ili aishi vyema katika ndoa.

Kassim kwa jinsi alivyoona tu alikuwa mkewe yupo njia moja kuondoka. Alivyomkuta na mabegi yake aliona kabisa kuwa atamkosa mke. Na yeye pia aliwahi kuambiwa na rafiki ya mkewe asuke au anyoe, la sivyo atamkosa mke.

"Wewe mwanamume ukilemaa nakwambia mke huna. Ipo siku ataondoka na kukuacha na dada yako mbaki mnatumbuliana macho. Havijawa ni shoga yangu, lakini kwa alichomfanyia yule dada sijakipenda. Lazima uongee na dada yako au ufanye kitu ambacho kitamaliza hili tatizo, vinginevyo jiandae kumkosa mke. Mimi siwezi kukupa ushauri wa kumkandamiza mkeo, au dada yako. Uamuzi unao mwenyewe kaka kusuka au kunyoa." Maneno aliyoambiwa na Fatuma, shoga ya dada yake yalijirudia tena kichwani mwake.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# REMA KUTUMBUIZA TUZO ZA BRIT

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria,Divine Ikubor, maarufu kama Rema, amechaguliwa kuwa miongoni mwa wasanii watakaotumbuiza katika tuzo za BRIT zinazotolewa nchini Uingereza.

Waandalizi wa tuzo hizo maarufu nchini humo walitangaza kupitia ukurasa wao wa mtandao wa kijamii Alhamisi asubuhi kuwa Rema atatumbuiza kwenye sherehe hizo.

Rema kupitia ukurasa wake wa Instagram alithibitisha kwa kuandika kwamba atakuwepo katika tuzo hizo za BRIT zitakazotolewa Machi 2, 2024.

Mwanamuziki huyo atakuwa msanii wa pili wa Nigeria kutumbuiza katika tuzo hizo, wa kwanza alikuwa Burna Boy aliyetumbuiza 2018.

# Kanye West presha tupu mtandaoni

ALBAMU mpya ya rapa maarufu wa Marekani, Kanye West, imeingia katika utata baada ya kuondolewa katika majukwaa ya kuuza muziki kimtandao.

Muda mfupi baada ya kuachilia albamu hiyo inayoitwa "Vultures 1," aliyoshirikiana na mwanamuziki Ty Dolla Sign, iliondolewa kwenye mtandao wa Apple Music na iTunes Alhamisi alasiri na kubakisha nyimbo chache pekee.

Wakati mashabiki wa mwanamuziki huyo wakiwa katika taharuki, muda mfupi albamu hiyo ilirejea kwenye majukwaa hayo ikiwa na jina la msambazaji mpya Label Engine, badala ya ile ya awali FUGA ambayo ilisema imejiondoa kufanya kazi na msanii huyo.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMKOMALIA TONEY
CHELSEA inavutiwa na mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 27, na fowadi wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson (19), kwa sababu chaguo lao la kwanza, mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen (25), anasakwa na Paris St-Germain. (***Standard***)

### MRITHI WA MBAPPE ASAKWA
PARIS St-Germain inamtaka mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 26, nyota wa AC Milan na mshambuliaji wa Ureno, Rafael Leao (24) ili kuchukua nafasi ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (25), ambaye anaondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu. (***La Gazzetta dello Sport***)

### GUIMARAES ANUKIA PSG
PSG pia wanataka kuziba pengo la kuondoka kwa Kylian Mbappe kwa kuwasajili kiungo wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26, na kiungo wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva (29). (***L'Equipe***)

### GRAY ATAJWA LIVERPOOL
LIVEROOL wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Leeds United na kiungo wa timu ya England ya vijana walio chini ya umri wa miaka 20, Archie Gray, huku Leeds United wakiwa na uwezekano wa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 ikiwa hawatapanda daraja hadi Ligi Kuu. (***Football Insider***)

### NETO KUWEKA REKODI WOLVES
MCHEZAJI anayelengwa na Arsenal, Pedro Neto, anaweza kugharimu zaidi ya pauni milioni 60, huku Wolves wakishikilia ada ya rekodi ya klabu kwa mshambuliaji wao wa Ureno mwenye umri wa miaka 23, ambaye pia anaizivutia Tottenham Hotspur na Liverpool. (***Standard***)

### MAIA AITAMANI EPL
KIUNGO wa kati wa Sao Paulo, Mbrazil Pablo Maia, mwenye umri wa miaka 22, ana shauku ya kutaka kuhamia katika Ligi Kuu England, huku Arsenal, West Ham na Fulham zikitajwa kumwania. (***Mail***)

### SUAREZ KUSTAAFIA MIAMI
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool na Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 37, amesema klabu ya Ligi Kuu Soka ya Marekani ya Inter Miami itakuwa timu yake ya mwisho katika maisha yake ya soka. (***AS***)

### CLARKE NJIA MOJA
MSHAMBULIAJI wa Sunderland, Jack Clarke, mwenye umri wa miaka 23 anaweza kuondoka msimu ujao kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo, baada ya klabu hiyo ya Championship kukataa ombi la Lazio ya Serie A dirisha la usajili la Januari. (***Sunderland Echo***)

### LLORENTE AKARIBIA ROMA
AS Roma inataka kumsajili mlinzi wa Leeds United na Hispania, Diego Llorente mwenye umri wa miaka 30, kwa mkataba wa kudumu baada ya kuonyesha kiwango kizuri alipokuwa kwa mkopo katika timu hiyo inayoshiriki Serie A. (***Yorkshire Evening Post***)

### ANDERSON KUTUA WEST HAM
JUVENTUS wamekutana na winga wa zamani wa West Ham, Felipe Anderson, huku Mbrazil mwenye umri wa miaka 30 akimaliza mkataba katika klabu ya sasa ya Lazio msimu huu wa joto. (***La Gazzetta dello Sport***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: ALONSO KOCHA BORA WA KIZAZI KIPYA

**LIVERPOOL,** England

**●●● Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool anaongoza kwenye orodha ya...**

JURGEN Klopp amemsifu, Xabi Alonso, ambaye ni mmoja wa walio mstari wa mbele kuchukua nafasi yake katika klabu ya Liverpool, akisema ni kocha "bora" wa makocha wa kizazi kipya.

Tangu Klopp alipotangaza mwezi uliopita atajiuzulu kuifundisha Liverpool mwishoni mwa msimu huu, Alonso, kiungo wa zamani wa Anfield kati ya mwaka 2004 na 2009, ametazamwa kama mgombea anayeongoza kuchukua nafasi yake.

Raia huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 42 ameiongoza Bayer Leverkusen kufikisha pointi tano kileleni katika Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), na timu hiyo imebakisha mchezo mmoja kufikia rekodi ya muda wote ya Bayern Munich ya michezo 32 bila kupoteza katika mashindano yote.

"Xabi anafanya kazi nzuri sana," alisema Klopp akiviambia vyombo vya habari.

"Hiyo ni huru kabisa ya ripoti zinazomhusisha Alonso na Liverpool. Kama ungeniuliza wiki nane zilizopita kuhusu Xabi Alonso, ningeenda: 'Oh Mungu wangu.'

**"Kama unamtaka Carlo Ancelotti, Jose Mourinho na Pep Guardiola, labda mimi sitaweza kufanya hivyo kwa miaka 20 ijayo. Sawa, labda Mourinho atafanya. Kizazi kijacho tayari kipo hapo na naweza kusema Xabi ndiye mashuhuri katika idara hiyo."**

Alonso, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA wakati alipokuwa Liverpool, yuko katika kazi yake ya kwanza ya ukocha mkuu baada ya kuinoa Leverkusen kuanzia Oktoba, mwaka 2022.

"Mchezaji wa zamani wa kiwango cha dunia, kutoka familia ya ukocha pia ambayo inasaidia kidogo, alikuwa kama kocha tayari alipokuwa akicheza," aliongeza Klopp.

"Soka analocheza, timu inazoanzisha, uhamisho aliofanya, ni wa kipekee kabisa. Nilicheza kwa muda mrefu kwenye Bundesliga na inavutia sana. Sio tu hesabu ya pointi bali na jinsi wanavyocheza.

"Leverkusen ina nafasi nzuri sana ya kushinda kombe. Unapotazama Ligi ya Europa, Leverkusen ni mojawapo ya wanaopewa nafasi kubwa zaidi kwa hivyo inaweza kuwa msimu kwa Leverkusen."

Wakati Klopp alisisitiza alipoamua kumalizia kukaa kwake kwa miaka nane Anfield hatakuwa na mchango wowote katika kuchagua mrithi wake, uidhinishaji wa Mjerumani huyo kwa shauku hauwezi kudhuru matarajio ya Alonso.

Alipoulizwa juu ya uwezekano wa kuwa kocha wa Liverpool baada ya tangazo la Klopp mnamo Januari, mwaka huu Alonso alisisitiza alikuwa akizingatia Leverkusen lakini akaongeza "nini kitatokea baadaye, sijui."

## HABARI MICHEZO

# POCHETTINO: SIJABADILISHA NAFASI YA ENZO UWANJANI



**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amesisitiza hajabadilisha nafasi ya Enzo Fernandez katika timu ya Chelsea licha ya mabadiliko makubwa ya kiwango kutoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina.

Mchango wa Fernandez umekuwa ukichunguzwa msimu huu na Pochettino amekabiliwa na shutuma matumizi yake ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 yamechangia moja kwa moja matatizo ya Chelsea.

Mifano kadhaa ya Fernandez kuchezeshwa nafasi ya juu kama mshambuliaji wa kwanza imeangaziwa na mashabiki kwenye mitandao ya kijamii.

Katika wiki za hivi karibuni, kumekuwa na mabadiliko dhahiri katika mchango wa Fernandez.

Sio tu amekuwa akihusika zaidi na maandalizi ya Chelsea, lakini nyota huyo raia wa Argentina ameangaza macho kwa bao, akifunga mara nne kwa mwaka 2024.

Alipoulizwa kama mabadiliko haya katika nafasi ya Fernandez ni ya kudumu, Pochettino alikanusha kubadilisha chochote na badala yake akasisitiza sasa yuko sawa kimwili kutoa mchango wake uwanjani.

"Wakati mwingine ni tofauti na jinsi tunavyoona vitu," alisema Pochettino.

"Siamini sasa anacheza kwa kina zaidi, nadhani siku zote tulifikiri ni mchezaji mwenye uwezo wa kujenga katika maandalizi yetu, tukimtumia yeye na ubora wake. Na kisha kufika kwenye eneo la tofauti na uwezekano wa kufunga."

# Mourinho aipa City, Madrid taji la UEFA

**LONDON,** England

JOSE Mourinho anaamini Manchester City ndio washindani wakuu wa taji la Ligi ya mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England msimu huu, lakini anatarajia Real Madrid itaoa ushindani mkubwa kwa taji la Ulaya.

City hatimaye walitwaa Kombe la Ulaya msimu uliopita, na kushinda mataji matatu na kumaliza msimu bora kabisa katika historia ya klabu hiyo.

Kikosi cha Pep Guardiola kinapigiwa upatu kutwaa tena Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia wakipania kuwa timu ya kwanza kushinda ligi kuu ya England kwa miaka minne mfululizo.


Wakati akifanya mahojiano na Rio Ferdinand, Mourinho aliulizwa utabiri wa washindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu ya England msimu huu.

"Ligi ya Mabingwa Ulaya, ningesema City au Real Madrid. Ikiwa mtu nje ya wale wawili atashinda, kwangu, itakuwa mshangao mkubwa," alisema.

"Ningependa Real Madrid kushinda tena kwa klabu na kwa Carlo Ancelotti. Sijui, Bayern Munich wanaweza kufanya hivyo na Paris Saint-Germain.

"Nikiangalia uwezo, nadhani City/Liverpool kwa Ligi Kuu, City/Real kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Wakati Mourinho hakushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu yake mitatu akiwa na Madrid, nafasi yake ilichukuliwa na Ancelotti, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa katika msimu wake wa kwanza pale Santiago Bernabeu na sasa anawinda Kombe lake la tano la Ulaya kama kocha.



# Arteta: Siwazuii makocha kuondoka

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesisitiza hatamzuia msaidizi wake yoyote kuchukua kazi ya ukocha sehemu nyingine, huku Norwich City ikimtaka Carlos Cuesta, kuinoa timu hiyo.



Vyanzo vimeiambia ESPN Norwich wamemtambua Cuesta kama mbadala wa kocha wa sasa, David Wagner, ambaye yuko chini ya shinikizo kubwa klabuni hapo.

Hakuna uwezekano wa Norwich kufanya mabadiliko ya mara moja lakini wanafikiria kutafuta mbadala wake kabla ya mwisho wa msimu au msimu huu wa joto, huku Cuesta mwenye umri wa miaka 28, akijijengea sifa ya kuwa mmoja wa makocha wakuu wa soka tangu ajiunge na Arsenal kutoka Juventus mwaka 2020.

Ben Knapper tayari ameondoka Arsenal na kuelekea Norwich na, katika nafasi yake kama mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, anaaminika kuwa ndiye anayechochea nia yao ya kutaka kumchukua Cuesta.

Bado haijawa wazi kama Cuesta atakubali kazi hiyo ikiwa angepewa.

Alipoulizwa kama atamzuia iwapo ataomba kuondoka, Arteta alisema Ijumaa: "Ikiwa ndiyo. Huwezi kufanya hivyo. Sitafanya hivyo, hapana.

"Pamoja na wafanyakazi pia, kila mtu anahitaji kuhisi kuna njia, kuna mpango wa maendeleo kwa kila mtu. Watu hawataki kufanya kitu kimoja kwa miaka mitatu, minne, mitano. Ni njia ya kuhamasisha watu wengine halafu uchunguze kwa sababu hujui kikomo cha mtu isipokuwa unamuweka wazi kwa mambo fulani.

"Nadhani udadisi ni sifa muhimu sana ambayo tunayo ndani ya wafanyikazi wetu wachanga na ambayo inawasukuma wengine.

"Sote tunahitaji nafasi. Nilipata nafasi wakati sikuwa na uzoefu wa kufundisha, kwanza Man City na hapa. Ninashukuru sana kwa hilo.

"Ni jukumu langu kutoa, unapoona vipaji, unapoona kiwango hicho cha shauku na shauku kuwapa nafasi pia kuonesha kile wanachoweza kutoa."

## Mabao ya 'usiku' tatizo Geita Gold

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold FC, Denis Kitambi, amesema wachezaji wake wanaonekana kukosa umakini katika dakika 10 za mwisho katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo nyota wake wamekuwa wakiruhusu mabao.

Mara baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kufungwa mabao 2-1, Kitambi alilia na safu yake ya ulinzi akisema wanakosa umakini, hali ambayo inawafanya wapoteze pointi.

Katika mechi ya juzi, Geita Gold iliruhusu bao la kwanza dakika moja kabla ya mapumziko, likifungwa na Gilbril Sillah huku goli la pili likiwekwa wavuni na Idd Nado dakika saba kabla ya mechi kumalizika wakati wao walipata bao la kufutia machozi likifungwa na Tariq Seif.

Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Geita Gold iliruhusu bao dakika tisa kabla ya mechi kumalizika likifungwa na Babakar Sarr na hivyo Simba kuondoka na pointi tatu.

Kitambi alisema wachezaji wake wamefanya makosa hayo katika mechi mbili zilizopita na pia amebaini mabao yote waliyoruhusu ni ya krosi.

"Mechi ya pili tunaruhusu goli katika dakika 10 za mchezo ni lazima tukifanyie kazi, ni ukosefu wa umakini, na nimeona pia katika mechi zote mbili pia mabao yote tunafungwa ya krosi, inabidi sasa tufanyie kazi, tunagalie ni namna gani tunajilinda dhidi ya krosi," alisema Kitambi.

Hata hivyo, kocha huyo ameonyesha kufurahishwa na kiwango cha wachezaji wake katika mechi ya juzi tofauti na walipocheza dhidi ya Simba.

"Leo (juzi), angalau tumeweza kumiliki mpira, wachezaji wangu 'mali' ilikuwa inakaa mguuni tofauti na mechi dhidi ya Simba ambapo walionekana wana wasiwasi, tunaangalia sasa tuendelee kujenga kutokana na hiki tulichokipata na kukiona," Kitambi alisema.

# SKUDU AFUNGUKA KUHUSU 'KUSUGUA' BENCHI YANGA

**Na Saada Akida**

WINGA wa Yanga, Mahlatse Makudubela 'Skudu' amesema hajakata tamaa na anaendelea kupambana kusaka namba katika kikosi cha timu kinachoendelea kusaka pointi muhimu ili kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Skudu, raia wa Afrika Kusini ameshindwa kupata namba katika kikosi cha timu hiyo kinachonolewa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Akizungumza na Nipashe jana, Skudu alisema ameshindwa kupata nafasi ndani ya kikosi cha kwanza kwa sababu ya ushindani uliopo lakini kamwe hawezi kukata tamaa na anaamini ataisaidia timu kila atakapopata nafasi ya kucheza.

**"Nitaendelea kujituma katika mazoezi na ninaamini ninatakiwa kuonyesha kitu kila na fasi ya kucheza nita kayopewa na kocha, bado nina nafasi kwenye timu, wakati uki fika nitaonyesha ubora wangu," alisema Skudu.**

Aliongeza anaimani na kiwango chake bado kipo vizuri kwa kusaidia Yanga kufikia malengo yao kwenye mashindano ya ndani na yale ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanayoshiriki.

Alisema morali ya wachezaji wa Yanga iko juu kwa sababu wanajipanga kuwapa furaha wanachama na mashabiki wao kila wanapocheza.

"Ni kweli ushindani wa namba ni mkubwa, kikubwa nitapambana kuhakikisha ninafanya vizuri na kusaidia Yanga kupata matokeo chanya, ninaimani nitaonyesha kiwango kizuri kila ninapopata nafasi ya kucheza.

Mashabiki wa Yanga wanapenda mpira jambo ambalo naliona ni zaidi ya familia kuichezea timu hii na niwaambie tu kuwa nitapambana kwa ajili ya kuyapata mafanikio makubwa zaidi na kuweka historia nyingine," alisema Skudu.

Aliongeza anaendelea kuongeza juhudi kwenye uwanja wa mazoezi huku akisema bado mechi zilizobakia kukamilisha msimu ziko nyingi.

Usajili wa nyota huyo ulifanyika kwa mbwembwe na jezi namba sita aliyopewa ambayo awali ilivaliwa na kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', ilionekana itaipa faida kubwa Yanga.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), wakijinoa kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki dhidi ya Afrika Kusini itakayochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *JKU yapunguzwa kasi Ligi Kuu Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya JKU SC imeendelea kupunguzwa kasi katika mbio ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Malindi SC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi jioni.

JKU SC walikuwa wa kwanza kuzifumania nyavu za wapinzani kupata bao dakika ya tatu kupitia, Abdallah Said wakati Malindi walisawazisha goli hilo dakika ya 57 kupitia Ramadhani Mponda.

Matokeo hayo yanaifanya JKU kusalia kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar wakiwa na pointi 40 huku nafasi ya pili ikishilikiwa na KMKM SC yenye alama 38 na Malindi SC yenye ikiwa nafasi ya 11 na alama zake 19.

Akizungumza baada ya kumalizika mchezo huo, Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali, alisema kutofanya vizuri katika michezo miwili mfululizo kumetokana na ushindani uliopo katika ligi hiyo hasa katika mzunguko huu wa lala salama.

Ali alisema kila timu wanayokutana nayo inacheza mfumo wa kujihami na kukamia ili kuhakikisha haipotezi mchezo.

Kocha huyo alisema mechi za mzunguko wa pili huwa ni ngumu kwa sababu kila timu inacheza kwa juhudi ili kufanikisha malengo yake waliyojiwekea wakati wanaanza msimu.

"Mzunguko wa pili ni mzunguko wa mapambano katika Ligi Kuu Zanzibar, ligi huwa ni ngumu mara mbili ya mzunguko wa kwanza, timu zinashuka uwanjani kucheza kwa kasi na zenye kuhitaji matokeo chanya, hivyo kosa moja tu ukilifanya linaweza kukuadhibu," alisema kocha huyo.

Aliongeza licha ya kupata bao la mapema, washambuliaji wake walipoteza umakini na kushindwa kuzitumia vyema nafasi mbalimbali za wazi walizotengeneza.

"Kama washambuliaji wangu wangekuwa watulivu, tungepata ushindi, walishindwa kumalizia kufunga nafasi ambazo walitengeneza, tutaendelea kurekebisha makosa kwa sababu bado tuko katika vitani," Ali aliongeza.

Hata hivyo aliwapongeza wapinzani wao kwa kucheza vizuri na kutovunjika moyo kutokana na kufungwa bao la mapema na badala yake walipambana na baadaye walifanikiwa kusawazisha.

Alisema anaamini wataingia dimbani tofauti katika mechi yao inayofuata dhidi ya Zimamoto itakayochezwa Februari 23, mwaka huu.

# Michezo

Jumapili Februari 18, 2024

Nipashe




Mourinho aipa City, Madrid taji UEFA UKU. 22

# Yanga haikamatiki

## Mabingwa hao watetezi watoa dozi nyingine kwa KMC huku Mudathir akizidi…

**Na Adam Fungamwango**

MABAO ya viungo, Mudathir Yahya na Pacome Zouzoua, yaliiwezesha Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro jana.

Kiungo mkabaji, Mudathir alifunga mabao mawili katika mchezo huo wa kwanza wa mzunguko wa pili na sasa amefikisha mabao sita msimu huu huku goli lingine la kiungo mshambuliaji, Pacome, raia wa Ivory Coast, pia lilimfanya kufikisha idadi kama hiyo.

Matokeo hayo yanawafanya mabingwa hao watetezi, Yanga kuendelea kujiimarisha kileleni katika msimamo wa ligi wakifikisha pointi 43 na kuicha KMC ikiwa nafasi ya tano na pointi 12 kibindoni.

**Beki wa kushoto wa Yanga, Nickson Kibabage, alitoa pasi mbili za mwisho za mabao hayo na kumfanya awe na 'asisti' nne katika ligi mpaka sasa.**



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya (kushoto), pamoja na straika wa timu hiyo, Clement Mzize wakishangilia katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro jana. Yanga ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

Yanga ilitimiza msemo unaosema biashara asubuhi, ilipoandika bao la kwanza katika sekunde ya 54 kupitia Mudathir ambaye kwa siku za karibuni amekuwa kama 'moto'.

Baada ya kuona wanaanzia mpira nyuma na kupasiana kwa karibu bila tahadhari na wakati mwingine kumrudishia kipa, Maseke, nyota wa Yanga waliwazingira KMC na Clement Mzize, alifanikiwa kuupokonya akiwa karibu na lango, mpira akampelekea mfungaji ambaye apiga shuti kali lililowababatiza mabeki, ukamrudia Stephane Aziz Ki, ambaye naye alijaribu, lakini kipa aliupangua, ukaenda kuangukia tena kwa kiungo huo kabla ya kuupachika wavuni kiulaini.

Baada ya bao hilo la 'asubuhi' wachezaji wa KMC walionekana kuchanganyikiwa na kufanya makosa mengi katika eneo lao la hatari na kama wachezaji wa Yanga wangekuwa makini wangemaliza kipindi cha kwanza wakiwa na mabao zaidi ya matano yale waliyofunga mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Agosti 23, mwaka jana.

Mzize peke yake alikosa mabao ya wazi, dakika ya tisa alipobaki yeye kipa, lakini akapiga shuti dhaifu lililoishia mikononi kwa Maseke, dakika ya 11, akiwa yeye na Maxi Nzengeli, wakikabiliana na kipa wa KMC, lakini mpira ukaenda nje, dakika ya 26, akiwa yeye na nyavu, akapiga nje, na dakika ya 34 akiwa pia jirani la lango tupu akapiga pembeni.

Kwa upande wake, Pacome, alikosa bao dakika ya 14, shuti lake likidakwa na Maseke.

KMC ilifanya mashambulizi yake dakika ya 10, wakati Awesu Awesu, alipotandika shuti kali lililowababatiza mabeki wa Yanga, kabla ya kudakwa na kipa, Djigui Diarra, aliyekuwa langoni kwa mara ya kwanza baada ya kurejea kutoka katika Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), akiitumika Mali.

Dakika ya 27, Fred Tangalu, akiwa nje ya eneo la hatari alipiga shuti kali lililotoka sentimeta chache langoni kwa Yanga, huku Diarra akiwa amechelewa kufika eneo la tukio.

Kipindi cha pili, KMC ilimtoa kipa wake, Maseke ambaye alionekana hayupo vizuri, akigombana na mabeki wake na nafasi yake ikachukuliwa na Denis Richard, lakini haikuwa dawa.

Mudathir alipachika bao la pili dakika ya 53, alipoutokea mpira wa krosi iliyopigwa na Kibabage, wakati mabeki wa KMC wakiusubiri kuokoa, mfungaji alitoka nyuma yao na kuukwamisha wavuni kirahisi tu.

Dakika sita baadaye, Pacome alisawazisha makosa yake kwa kuiandikia Yanga bao la tatu, akiunganisha kriso ya Kibabage kutoka wingi ya kushoto.

Ni kama KMC walizinduka baada ya mabao hayo matatu kwa sababu walianza kumiliki mpira, hasa Awesu ambaye alionekana yuko katika kiwango cha hali ya juu.

Straika mpya wa Yanga, Joseph Guede, aliyesajiliwa hivi dirisha dogo la usajili, alikosa mabao mawili ya wazi, moja akigongesha mwamba alipopiga kichwa mpira uliotoka kwa Musonda.

# Simba yatanguliza 'wauaji' Asec CAF

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanavuna pointi tatu muhimu, mabosi wa Simba wanaamini kiungo wao, Aubin Kramo, atasaidia kuhakikisha 'hesabu' za kuwafunga Asec Mimosas katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika zinakamilika.

Kramo, nyota wa zamani wa Asec Mimosas na Mratibu wa Simba, Abbas Ally, wametangulia nchini Ivory Coast kuweka mazingira sawa ya ushindi kwa timu yao.

Taarifa kutoka Simba zinasema Kramo na kiongozi huyo wanaondoka nchini leo kwa ajili ya kwenda kufanya maandalizi ya kuipokea timu pamoja na kuweka mikakati mingine ya ushindi vyema.



Chanzo chetu kilisema kikosi cha Simba kitaondoka nchini kati ya Jumatatu au Jumanne kuelekea nchini humo kwa ajili ya mchezo wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Felix, Houphouel-Boign.

"Kramo atakuwa sehemu ya maofisa wa awali watakaotangulia Ivory Coast kabla ya msafara wa timu kuondoka, nyota huyo anafahamu sehemu zote za nchini humo, pamoja na kuwafahamu vizuri wapinzani wetu (Asec Mimosas), tunaamini atatusaidia kutuongezea taarifa muhimu," kilisema chanzo hicho.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alisema baada ya kukamilika kwa mchezo dhidi ya JKT Tanzania, alifanya kikao na wachezaji wake kuweka mikakati ya ushindi watakapowakabili wenyeji Asec Mimosas.

Benchikha alisema anahitaji kwenda kuvuna pointi muhimu na tayari amepokea taarifa muhimu kuhusu wapinzani wao ikiwemo mbinu za kifundi wanazotumia pia akifahamu ubora na madhaifu yao.

"Ni mechi muhimu kwetu kushinda, tumeanza kufanyia kazi ubora wa Asec Mimosas, lakini pia kusahihisha makosa tuliyoyafanya katika michezo iliyopita, tutapata muda wa kufanya maandalizi mazuri na kila mchezaji anatambua umuhimu wa mchezo wetu ujao," alisema Benchikha.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanalishukuru Shirikisho la Soka Tanzania kwa kuahirisha mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar kutokana na kibarua 'kigumu' walichonacho cha kuivaa Asec Mimosas.

Alisema changamoto za safari ni moja ya sababu ambazo TFF na Bodi ya Ligi (TPLB) wamezingatia na kuahirisha mechi hiyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >